


TAFAKA



ORI



THE OPEN SOCIETY INITIATIVE 
FOR EASTERN AFRICA 

KUKUZA DEMOKRASIA

MAHIRI NA VUMILIVU

MAPENZI YETU

8

Mapenzi yetu ndio kichocheo cha kazi yetu.

Inaamsha ari ya kufanya kazi bunifu kwa akili zaidi. Uchu huu unatupatia nguvu zaidi, mabadiliko, na ustahimilivu wa kufanya kazi kwenye mazingira magumu na yenye changamoto, mapenzi yetu yanafanya tusimame bila woga na kuhimili hatari na kutokua na uhakika.

HAKI

10

Haki inawakilisha yote tunavyosimamia.

Lengo letu ni kuhakikisha kila mtu – kwa ujumla na sio kinadharia wanapata haki sawa kushiriki kikamilifu katika jamii na kupata haki na 'hakisawa' kutoka kwa serikali na jamii.

USAWA

16 | 20

Tunafanya kazi kwa msingi wa binadamu WOTE wana-haki ya kupata haki za msingi na kupata fursa sawa na rasilimali.

Watu walioko kwenye makundi yaliyotengwa na wachache mara nyingi hunyanyapaliwa na kuteswa. Sisi huwapa usaidizi katika mada'i yao ya kupata haki za kibinadamu minghaiiri ya jinsia, rangi, kabila, dini, uzao, umri, ulemavu, mu-elekeo wa kijinsia, ama misingi mingine. Ukizingatia uenezi wa mifumo dume na mifumo ya kijamii ambayo inawakandamiza wasichana na akina mana, tunasimama kidete ku-fanikisha usawa wa kijinsia.

KUSHEREHEKEA UTOFAUTI

24 | 28

Tunasaidia katika jitihada za kusheherekea na kushajisha nguvu za utofauti wetu na kukuza uelewano katika tofauti zetu.

Tunaishi kwenye jamii yenye watu wa kila aina watokao kwenye misingi tofauti, imani tofauti na mienendo tofauti ya maisha. “Ni sisi” kwasababu “wao ni” and “wao ni” kwasababu “ni sisi”: wale wote ambao wanataka kushirikiana na kutafuta umoja tuko pamoja nao.

UBUNIFU NA UVUMBUIZI

32

Tunajipa changamoto kufikiria tofauti – njia mbadala, mawazo mbadala, ufahamu pamoja na washirika – kupanua mipaka ya uwezekano.

Mabadiliko yanaweza kuja tu kwa kutafuta nafasi kwa ubunifu, na ikiwezekana kuwa tayari kuingia matatani. Tunapaswa kutoogopa kufeli wakati kuna fursa murwa ya mafanikio. Hakika, tunathamini mafunzo na ukuaji kiakili.

UADILIFU

40

Uadilifu unamaanisha kufanya tunayoyanena.

Tunawajibika na kujibu mienendo yetu (ya kutenda na kutotenda) kwa wote. Tunadumisha maadili mema na utaalumu wa hali ya juu katika miingiliano yetu. Kwetu sisi, uadilifu ni kujenga mahusiano halisi kupitia heshima na hali ya usawa.

MSHIKAMANO NA UMOJA KAZINI

46

Sisi ni timu ambayo inafanya kazi kwa ushirikiano na kwa umoja.

Uelewa wetu, uwajibikaji na ushirikiano umezalisha nguvu ya kufanya kazi kwa uhakika. Miingiliano yetu daima huwa ya adabu na endelevu. Tunafanya kazi yetu kwa utulivu na ucheshi mkubwa. Tunasimama na wafanyakazi wenzetu wakiwa na wakati mgumu.

TAFAKARI

WWW.OPENSOCIETYFOUNDATIONS.ORG

Mkurugenzi Mkuu BINAIFER NOWROJEE

Waandishi EMMA DAY
UMRA OMAR
JOANNA OYEDIRAN
DON BOSCO MALISH

Wahariri BINAIFER NOWROJEE
UMRA OMAR

Mhariri msaidizi CLEMENTINE LOGAN

Mkurugenzi wa ubunifu ASSEGID GESSESSE
Mpangilio na ubunifu ISSA ABDUL

Tafsiri NICODEMUS MINDE

TOVUTI NA MAONI

www.opensocietyfoundations.org | info@osiea.org

NAIROBI | KAMPALA | DAR ES SALAAM | JUBA

Chapa na:
OSIEA
S.L.P 2193-00202
Nairobi, Kenya
+254(20)387-7508

© OSIEA.

Pasipokuwa na vizuizi, unaweza kuchapisha tena kazi yetu. Shirika la OSF linaamini kwamba lengo lao linaendelezwa endapo kazi tunazozisaidia na kubuni zinawekwa wazi na inapatikana kwa umma

TAFAKARI

MAPENZI YETU



SISI NI NANI?

“MAPENZI YETU NDIYO KICHOCHEO CHETU...”

Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) inakuza demokrasia mahiri na jumuiishi.

OSIEA ilianzishwa 2005 na imekua hodari katika kuhamasisha uwazi, mazungumzo ya kinifu kuhusu masuala yenye umuhimu katika umma. Tunasaidia watu binafsi na makundi kushiriki kwenye masuala yanayowagusa ilikudai huduma bora na uwajibikaji kutoka kwa viongozi na taasisi zao. Tunatoa mikopo isiyo na riba, tunaandaa mipango yetu, na kukuza majadiliano/midahalo muhimu ya masuala ya umma. OSIEA ni mshirika wa mtandao wa kimataifa wa taasisi ya Jamii Wazi (Global Open Society Foundations Network).

Kazi ya OSIEA hufanywa kupitia ujumuisho wa nchi mbalimbali na mipango mahususi. Tunakuza tawala za

kidemokrasia/haki na haki za kibinadamu, kuheshimu utawala wa sheria na kulinda haki za waliotengwa.

Jukumu kuu la OSIEA ni kukuza hizo sauti na maadili wazi katika jamii. Tunasaidia watu binafsi, mashirika, miungano, mashirika ya kiharakati, na mashirika ya kiserikali. Hatuna fikra yabisi kuhusiana na mawakala wa madabiliko Afrika Mashariki. Sauti za haki hupatikana kotekote.

Tunajijumuisha na mipango inayohusisha mashauriano na kujukuika. Tunashirikiana na makundi yaliyotengwa na jamii; wale walikuwa karibu na dhuluma, unyanyapaa na kutengwa. Hii inamaanisha wakati mwingine tunajihusisha na maswala ambayo wengi hawawezi jiingiza; tunachukua tahadhari ili kuhamasisha. Tunamini kwamba watu wote ni sawa.

Ndani ya OSIEA, jinsi tunavyofanya kazi zetu ni muhimu kama kazi yenyewe. Kama timu inayoendeshwa na misingi, matendo yetu, maneno yetu, na tabia yetu ndani na nje ya ofisi ni kielelezo cha mstakabali wetu katika kanda

hii. Misingi inayosimamisha shirika letu ndio kioo cha jinsi tunavyofanya kazi yetu. Msisitizo unawekwa kwenye uadilifu, uwajibikaji (miongoni mwetu na kwa wengine), kushereheka tofauti zetu na ushikamano. Kwa kutumia, mbinu ya maswali ya uthamini (Appreciative Inquiry) tunafanya kazi ilikujenga utamaduni wa nguvu unaotathmini ubora wetu, katika utendaji na matokeo.

Tunazingatia uwezekano; swali ni muhimu kuliko jibu. Mafunzo endelevu na uvumbuzi ndivyo vipaumbele vya timu yetu kwa ubunifu kushughulikia changamoto za ukanda huu. Kwa mujibu wa mazingira ya kazi yetu, OSIEA lazima ibaki nyumbufu na iwe na uwezo wakujinyumbua haraka ili tubaki na maana.

Mwisho, tunapata mamlaka yetu kupitia heshima na uaminifu kutoka kwa washirika wetu na wenzetu.

Hii ndivyo tunafanya na kwa mapenzi na kwa urahisi ndivyo tunavyofanya.

Binaifer Nowrojee
Mkurugenzi Mkuu.

HAKI



KUKABILIANA NA MAKUNDI YA KIHALIFU KWENYE NGAZI YA KIJAMII KENYA

Serikali ya Kenya kwasasa ime-tekeleza mpango kabambe wa mageuzi kwenye idara ya polisi. Mpango huu unajumuisha mbinu mbalimbali zikiwemo, maendeleo ya usimamizi wa polisi kwenye sehemu ambazo hamna usimamizi wa polisi, kujenga upya miundo mbinu ya idara ya polisi kwajili ya ubora wa uwajibikaji pamoja na kuboresha mahusiano ya polisi na jamii. Mbinu hizi huenda ukabadilisha idara ya polisi kuwa ambayo haiwajibiki na sheria na watu na kuwa sikivu kwa matakwa ya watu wa kawaida. Mageuzi haya hatimaye yatawapatia fursa jamii kuboresha hali ya usalama wao kuinga makundi ya kihalifu kushika uskani.

Jamii Wazi Ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) pamoja na Kitengo Cha Kuinga Uhalifu na Vurugu cha Jamii Wazi (Open Society's Crime and Violence Prevention Initiative) wanasaidia mipango ya kukuza mbinu changanishi za kuondoa uwajibikaji wa kusimamia ama kupunguza vurugu kutoka kwenye wigo la polisi na idara ya haki ya uhalifu, na kuiweka kwenye mikono ya wananchi waliowezesha.

OSIEA inashirikiana na Jukwaa la Usalama (Usalama Forum), ambalo ni muungano wa mashirika kumi na nne ambayo sio ya kiserikali kwenye maeneo lengwa manne; Kirinyaga, Mtwapa, Kisii, na Eastleigh. Jamii hizi huwakilisha hali mbali

mbali za uhalifu na vurugu Kenya. Kila jamii inashida zake za kipekee.



Mjini Kirinyaga, makundi ya vijana, sana sana ya wanaume, yamefika na kuchukua hali ya utupu na wanaendelesha kwa upande mmoja kundi halali la kipolisi ndani ya jamii, na kwa upande mwingine, kama wanamgambo chipukizi, wanaziba pengo lililoachwa kwenye utoaji wa usalama na mbinu zao za haki za kimgambo. Wanaachama wa makundi haya mara nyingi hujihusisha kama waendesha pikipiki. Wao ni kinyume cha kikundi kilichopoteza umaarufu cha Mungiki ambacho hutawala kwa mabavu sekta za huduma zisizo halali mjini Kirinyaga na eneo zima la nyanda za kati za Kenya mpaka walipofumuliwa kwa ubavu.

“Kikundi cha vijana” kama wanavyopenda kutambulika, huthibiti kwa nguvu huduma za usalama mtaani. Wanasimamia mahakama zao za kimtaa, ambazo hufaamika sana kama “The Hague” baada ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) iliyoko Uholanzi. Mahakama yao ya Hague iko chini mti wa mkuyu. Hapa watuhumiwa wanapewa adhabu mbalimbali zikiwemo ad-

habu ya kifo ama kukatwa viungo vya mwili. Kwasasa kutokana na mbinu hii, ya usimamizi wa usalama; eneo hili lina kesi kidogo za uhalifu na vurugu zinazoripotiwa katika jamii hii, Jukwaa la Usalama (Usalama Forum) linafanya kazi pamoja na hilo kundi la vijana kuzalisha itifaki mpya ya usalama kwa jamii. Uongozi wa kundi hili wanabuni mpango ambao utakuza mdahalo miongoni mwa jamii utakao husisha mchakato wa kipolisi kwenye jamii na kukacha dhana za kimgambo.

Kwenye eneo la Pwani la Mt-wapa, ukatili wa kijinsia unazidi kuongezeka kwasababu ya matumizi ya dawa za kulevya na ukatili miongoni mwa wapenzi. Ni kawaida kwa wasichana wenye umri mdogo kama 12, kubakwa na kudhaliliwa kimapenzi halafu familia zao kupanga waolewe na watuhumiwa hao wa ubakaji ili kulinda heshima yao na kukwepa sheria kwa watoto wao.

Haya yakitokea, polisi wanalazimika kusitisha upelelezi wao. Jukwaa la Usalama linafanya kazi na jamii ya Mt-wapa kujenga makubaliano andishi kuhusiana na matumizi ya dawa hatari za kulevya na kushirikiana na polisi.

Kisii wanakabiliwa na uhalifu na vurugu mbali mbali zikiwemo ghasia za hapa na pale, ukatili wa kijinsia na malumbano makali ya familia kuhusiana na mashamba, wizi na uharibifu unalenga mashine za kutolea hela, na udhalilishaji kimapenzi kwa watoto. Wahalifu wengi ni vijana wenye umri kati ya 18 hadi 30. Genge liitwalo Sungu Sungu hivi karibuni limekua na kuanzisha mfumo wa usalama kwenye mitaa ya wauza ngono pamoja na maeneo maalumu ya kupanda na kushusha abiria wa pikipiki. Pia wanajihusisha na mpango bandia wa ulinzi wa kijamii kwenye jamii hizi, kundi hili lime-watia watu hofu; wao ndio sheria. Kwasasa wanawatia wahalifu adhabu. Jukwaa la Usalama limekua likishirikiana na kundi hili na washikadau wengine muhimu kuzalisha mbinu mpya ya ushirikiano kwa ajili ya usimamizi wa usalama. Kuna kama pikipiki 10,000 na zaidi ya teksi 1,000 pamoja na magari binafsi na magari ya usafiri ambayo hayadhhibitiwi. Jukwaa la Usalama pia linashirikiana na vitengo vya mamlaka za mitaa, biashara za mitaa, hospitali na idara ya polisi kuzalisha mifumo mipya safi na salama za usimamizi wa trafiki.

Makundi ya kimgambo pia hutawala vitongoji vya Nairobi kwenye eneo la Eastleigh ambalo ni makazi kwa idadi kubwa ya jamii ya Wasomali pamoja na wakimbizi na wahamiaji kutoka nchi jirani iliyokumbwa na vita ya Somali. Kundi la Sitaki Kujua (I don't want to know) lime-thibiti mtaa wa First Street na wamiliki wa biashara kwenye mashambulizi na wizi. Wana-fahamu wazi kwamba wami-liko wa biashara wakiosomali hawatendewi haki na mam-laka na hivyo kwa nadra sana huripoti visa vya wizi kwa polisi na hupendelea uwasil-ishaji wa haki mbadala uit-wao Maslah huko Eastleigh. Kundi lingine la kimgambo ambalo husishwa na uhalifu wa kimabavu, linajumuisha sana sana vijana wadogo wakiume wakiosomali ambao wamefukuzwa kutoka mataifa ya Magharibi kama wasiostahili hadhi ya ukim-bizi. Idadi kubwa ya wakim-bizi na wahamiaji, wakiju-muishwa wale waliochini ya wasimamizi Shirika la Umo-ja wa Kimataifa linalosima-mia wakimbizi (UNHCR) na wale ambao hadhi yao hai-julikani wana athari kubwa kwenye mshikamano na shughuli za kiuchumi za kijamii. Mbinu za kipolisi ni za kimabavu na huchuku-liwa kama ubaguzi na watu wenye asili ya Kisomali.



HAKI

Kwenye jamii zote hizi mbinu ya Jukwaa la Usalama imekuwa ya ushirikiano, ambao unaoshirikisha watu wote muhimu kwenye jamii ambayo ni wadau kwenye usalama na ulinzi. Ushirikiano huu huleta sekta za umma, idara ya polisi, viongozi wa makundi haya ya kimgambo, asasi za kijamii, pamoja na viongozi wa ta-wala za mitaa. Jukwaa la Usalama halafu hufanya kazi na jamii kutengeneza timu ya kukinga wananchi ambao huongoza jamii kwenye kaguzi pana za usalama ili kutambua masuala muhimu. Pia huandaa makundi ya kujadiliana, huandaa watoa habari maalum, na huandaa majadiliano ya moja kwa moja na matembezi kupitia kwa shughuli hizi, ushirikiano unatengenezwa baina ya watu ambao mwanzo hawakufanya kazi pamoja.

MBINU ZA KIJAMII ZA KUZUIA UHALIFU EASTLEIGH

Moja ya eneo lenye heka heka nyingi, na hatari kabisa kwenye mtaa wa Estleigh ni karibu na kanisa la Mt. Te-

resa. Kanisa hili lipo kwenye njia panda ya barabara kuu mbili za kuelekea Eastleigh; Barabara ya Jogoo na Barabara ya Juja. Kwenye njia panda hii, watu wanakabwa na wezi wa mabavu na aina nyingine za uhalifu zimekithiri kutokana na giza. Haya yalithibitishwa wakati wa matembezi yetu kwenye jamii hii. Kupitia mkakati wa haraka wa mafanikio, kundi la kuzuia uhalifu, ikiwemo, Jamii ya wafanyibiashara wa Eastleigh, Chama cha Wakazi, Halmashauri ya Jiji, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) na chifu wa eneo hili lilianzisha mpango wa kuweka taa kwenye mitaa na katika kanisa la Mt. Teresa. Wakazi wa eneo hili wamethibitisha kwamba kuwepo kwa taa hizi kumesaidia kupunguza uhalifu kwenye mitaa hii, hadi sasa wale ambao hufanya uhalifu huu inaaminika wameanza kufanya hujuma na kuharibu taa na nyaya.

Mipango mingine inaendelea inayotokana na ushirikiano na uwepo wa timu ya kuzuia uhalifu na inahusisha ukarabati wa barabara ambayo itachangia katika kui-marisha usalama kwenye jamii hii. Washiriki wote wanatambua kwamba ili kuwa na usalama na ulinzi kwenye jamii ni lazima wafanye kazi pamoja na kusaidiana katika majukumu yao.

MACEUZI KWENYE IDARA YA POLISI KUTOKA CHINI HADI JUU

Kote nchini Kenya, imani ya wananchi kwenye idara ya polisi imezoroteshwa na hali ya juu ya ufasidi miongoni mwa polisi na uhalifu, na kuenea kwa dhana kwamba polisi wenyewe ni washirika katika uhalifu. Pamoja na kupanda kwa matukio mengi ya uhalifu, Kenya imeshuhudia kuuwawa kwa watu kiholela pasipo na idhini ya kisheria na polisi katika miaka ya hivi karibuni. Baada ya kuzidi kuilaumu na kuitenga idara ya polisi, Jukwaa la Usalama kwa makusudi wanashirikiana na maofisa polisi kwa kufanya midahalo ambayo polisi wanapewa fursa ya kueleza matarajio yao pamoja na hofu zao, na umma wanachangia maoni yao kuhusu mienendo ya polisi. Mikutano hii inahusu kutafuta msimamo jumuishi ili kufanikisha haki za kibinadamu na utekelezaji wa kipolisi, ambayo inawezekana wakati kuna upanuzi katika majadiliano. Kabla ya Jukwaa la Usalama kuingia katika jamii hizi, hamna mtu aliyetaka kuzungumzia masuala ya makundi ya kimgambo ama kusema polisi

walikua sehemu ya tatizo. Kwasasa wanaweza kuzungumzia haya kwa ujarisi.

KUSHIRIKIANA NA SERIKALI YA KENYA

Mnamo Februari 2012, Taasisi ya Utawala Kenya (KIA) ilimaliza somo lake la kwanza la kuzuia uhalifu na vurugu. Wakishirikiana na OSIEA. Wahitimu hao walijumuisha kama watumishi wa umma, polisi, maafisa wa serikali za mitaa na wafanyikazi wa jamii hamsini, kutoka kwenye semina hii ya kwanza ambayo ilichochea fikra mpya kwenye masuala ya kuzuia uhalifu na ikawapata chngamoto wanafunzi kuondoka kutoka kwenye dhana ya kawaida ya kutekeleza na kudhibiti uhalifu. Chuo cha USIU imesimamia ukuzaji wa mtaala ambao ulileta pamoja wawezeshaji 23 kutoka kote ulimwenguni. Kuna furaha kubwa kuhusiana na mafanikio ya ushirikiano huu wa kipekee pamoja na serikali ya Kenya.

MWAADA MPTA WA MSAADA WA KISHERIA

OSIEA pia imeshirikiana na Kamati ya Kimataifa na Wanasheria wa Kenya (ICJ-

K) ili kuwezesha tathmini ya mswaada wa msaada wa kisheria wa kitaifa. ICJ-K inamahusiano ya karibu na Mpango wa Kitaifa wa Msaada wa Sheria (NALEAP) uliopo chini ya Wizara ya Sheria. Msaada wa fedha usiokuwa na riba uliotolewa ili kuleta waataalum wa msaada wa sheria wakiitaifa na ukanda huu ambao walitathmini mswaada huu na kutoa mapendekezo ambayo yangeboresha mswaada huo.

MIKAKATI YA KISHERIA

Palikua na taharuki Kenya mnamo Januari 2012 wakati Mahakama ya kimataifa ya uhalifu (ICC) walipohititisha mashtaka dhidi ya vigogo wanne. Uamuzi huu ni hatua muhimu katika kutokomeza kutojaliwa kwa sheria nchini Kenya. Nchini, serikali imefanya kidogo sana kutafuta haki ya wahanga wa machafuko ya baada ya uchaguzi ya mwaka 2007. OSIEA pamoja na Jamii Wazi ya Haki (OSJI), wakishirikiana na vikundi vya Kenya wanasukuma kwa makosa yakimataifa yaliotendeka miaka mine iliopita yaletwe mbele ya mahakama ya Kenya.

Kupitia mfumo unaofahamika kama mbinu-shirikishi

(Complementarity), ushirikiano huu umetambua maeneo matatu ya muingiliano; mikakati ya kisheria, ulinzi wa mashahidi, na sera za fadia kwa wahanga.

USAWA |



HAKI ZA KINAMAMA

Jamii Wazi wa Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) na Jamii Wazi ya Mpango wa Kimataifa Wakinamama wanaisaidia mipango ya kukuza uwezeshaji wa kinamama na usawa wa kijinsia. Ijapokuwa harakati za haki za kinamama umefanikiwa pakubwa, akinamama na wasichana Afrika Mashariki bado wanakumbwa na hali ya juu ya ubaguzi na dhuluma. Udhalilishaji wa kinamama unajumuisha dhuluma za kimapenzi na dhuluma za kinyumbani pamoja na kisheria za mila na kitamaduni ambazo hubagua akinamama. Viwango vya vifo vya uzazi vipo juu sana na wakinamama wanayimwa fursa ya kujiamulia masuala yya afya ya uzazi pamoja na yale yanayohusu jinsia.

Masuala ambayo OSIEA amesaidia inajumuisha mipango ya kuhakikisha sauti za kinamama kwenye mageuzi ya kikatiba na sheria; kuwawezesha akinamama walioathirwa na vita wajenge upya maisha yao; kukuza upatikanaji wa haki kwa akinamama; na

kurekodi dhuluma kama kufanya tasa kwa akinamama waathiriwa wa ukimwi.

KUWAWEZESHA AKINAMAMA WAATHIRIKA WA VITA KASKAZINI MWA UGANDA

Kwenye kijiji cha Balonyo, kwenye eneo la Lira lilipo Kaskazini Uganda, wananchi bado wanakumbukumbu za mauaji yaliowaangamiza jamii yao Februari 21, 2004, wakati wa vita baina ya serikali ya Uganda na waasi wa Lord's Resistance Army (LRA). Waasi walikumbana na majeshi ya serikali na wakafanikiwa kuwazidi nguvu na kuwashinda. Walishambulia kijiji hichi na fimbo na bunduki wengine waliwanyonga watu kutumia mikono yao na kuwatupa kwenye moto. Waliofanikiwa kutoroka walirudi siku iliyofuatana kuhesabu miili 301 iliyoachwa chini. Asili mia themanini ya wanakijiji waishio Balonya walikua ndugu wa wale waliofariki kwenye mauaji hayo.

Mauaji haya ni moja wapo wa matukio mengi ya vurugu zinazotokea kaskazini Uganda wakati wa miaka ishirini ya vita, ambayo hatimaye iliisha 2007. Wakati wa vita serikali iliwaamisha watu wote wa kaskazini Uganda kwenye makambi. Waasi wa LRA walitisha kambi hizi kwa kuwateka nyara watoto kutoka kwenye vitanda vyao usiku na kuwafanya wapigane kama askari watoto, na wanawake wengi walidhalilishwa kimapenzi na wanajeshi wa Uganda ambao waliwekwa mahususi kuwachunga. Tangu vita viishe manamo 2007, serikali imekuwa ikiwarudisha watu kwenye makao yao ambayo waliacha miaka ishirini iliyopita

Kuna matatizo makubwa ya kijamii kwenye eneo hili lililotoka kwenye vita. Kwani watu wanaishi kwenye limbwi la umaskini. Kizazi kizima cha wanaume kinachukua muda wake mwingi wa kazi kwenye jeshi ama wakiishi kwenye makambi ya watu wali-ofurushwa kwenye makazi yao wakitegemea misaada. Wakati vita vilipoisha, wengi wao waliachwa na msongo

wa mawazo kutokana na yaliotokea vitani, wengine hawana ajira, na wasiokua na dira maishani. Msongo huu wa mawazo umesababisha ueneaji wa uraibu wa ulevi miongoni mwa wanaume wengi pamoja na visa vingi vya kujinyonga, unyanyasaji wa nyumbani na udhalilishaji wa mapenzi kwa wanawake na watoto. Kwa wanawake, msongo huu wa mawazo utokanao na vita umezidishwa na vitendo vya dhuluma za kimapenzi ma kijinsia ndani ya jamii zao. Wakazi wa Kaskazini mwa Uganda wanahisi serikali ileshindwa kuwasaidia kujenga upya jamii zao baada ya vita.

UWEZESHAJI WA JAMII

Shirika la Kuwezesha Amani na Maendeleo (FAPAD) linafanya kazi na wanakijiji wa Balonyo kuandaa midahalo ya kijamii na kusaidia wanakijiji kurudia hali yao ya maisha kwa kuwawezesha kuilazimisha serikali kusikiliza shida zao.

Wakati wa vita, jamii nzima zilifurushwa kutoka kwenye makazi yao na kuwekwa kwenye makambi, na mifumo ya kitawala iliporomoka pamoja na mifumo ya kitamaduni, hivyo kuacha mwanya kwenye mifumo mizima ya

kutawala. Shirika la FAPAD linafanya jitihada kuwawezesha wale wanaorudi kutoka kwenye vita kujenga upya miundo na mifumo ya kijamii pamoja na kuishirikisha serikali kwenye masuala ambayo inawahusu kama vile ukarabati, ujenzi na maendeleo.

Wafanyikazi wa FAPAD huwatembelea wanakijiji kila wiki na huwahabarisha kuhusu haki zao kisheria na kuwasaidia katika shida zao. Wanakijiji hukutana mara kwa mara na wakati mwingine huwaalika viongozi wa kisiasa ili wawaulize maswali na kufanya wawajibike.

UWEZESHAJI WA AKINAMAMA

Akina mama wa Mon Pae Yot kwenye kijiji cha Kalongo wamejipanga kwenye vikundi ambavyo hukutana kwa wiki chini ya kivuli cha moja wapo wa miembe. Akinamama hao wana mfuko wa akiba na mpango wa mkopo ambao wao huchangia kiwango kidogo kila wiki. Wana uwezo waku-kopa kutoka kwenye mfuko huu kwa matumizi kama karo za shule ama kianzilisho cha biashara ndogo ndogo. Kikundi cha kinamama wa Mon Pae Yot ni moja wapo wa vikundi 200 vya kinamama ambavyo Cha-

ma cha Parokia ya Kalongo (FOKAPAWA) hushirikiana kaskazini mwa Uganda, na wengi wao wanamipango kama hii jumuiya ndogo ndogo za akiba na mkopo (viroba).

Hapo awali mume wangu angeza shamba bila kushauriana nami na watoto, na hata ukoo usingeja kuhusu hili. Angeza shamba lote na kulewa. Lakini tulipojiunga kwenye kikundi cha akinamama, tulielimishwa kuhusu umuhimu wa majadiliano na hivyo nilikaa naye chini na kujadiliana kuhusu umuhimu wa yeye kushauriana nami kabla hajauza shamba. Kwa sasa anapotaka kuuza shamba anaomba ushauri wangu na tunakaa chini kujadiliana pamoja na watoto na hujadiliana pia kiasi cha fedha ambacho tutauza shamba. Hapo awali sikuwa nafahamu lolote kuhusiana na shamba na kwasasa ninauelewa na mara ya mwisho tulipouza shamba tulizungumza na kukubaliana kuhusu bei na tukaweza kutumia fedha hizo kuwapeleka watoto wetu shuleni. Kwasasa ninahisi kwamba mimi ni mwanamke na nina haki ya kusikilizwa na uhusiano wetu umeimarika

Agoro Santina, mwanachama wa kikundi cha akinamama wa Mon Pae Yot

Vikundi hivi vya akinamama pia husuluhisha matatizo kwenye jamii, hungilia kati kwenye kesi za unyanyasaji wa nyumbani, na hushirikiana na polisi kutatua kesi za ubakaji na unajisi. Pia vinaelimisha wasichana kubaki shuleni badala ya kuchagua ndoa za mapema.

Kikundi cha akinamama wa Gulu cha Maendeleo ya Kiuchumi na Utandawazi (GWED-G) kimekua kikihamasisha vikundi vya akinamama kuanzisha michezo ya kuigiza ili kuelimisha jamii kuhusu haki za kibinadamu. Akinamama huigiza jinsi ul-evi wa mabwana zao ambao huja nyumbani na kuwadhalilisha wake zao, walimu wakajaribu kuwadhalisha kimapenzi wanafunzi wao, na polisi wanaposaka rushwa. Maigizo hayo huwa ya kuchangamsha, yanachekesha na huvutia umati mkubwa wa watu, na huishia na ujumbe mzito wakati, kupitia igizo, wadhalimu kwenye kila tukio wanaletwa mbele ya haki.

Mmoja wa akinamama walieleza kwamba moyo yao hupata amani na hivyo husambaza moyo wa amani kwenye jamii nzima. Wawili wa wanawake hao walifanikiwa kuwa madiwani na kwasasa wanapigia upatu haki za kinamama ndani ya halmashauri.

UPATIKANAJI WA HAKI

Kikundi cha GWED-G kimetoa mafunzo kwa wale wanaojitolea kwenye masuala ya haki za kibinadamu, wale wanaofundisha watu kuhusu haki zao, na pia husaidia kufanya upelelezi wa kihalifu, hususan ule unaohusu dhuluma za kimapenzi na kijinsia. Wasaidizi katika mpango huu huripoti na kuwasilisha visa vya unajisi na ubakaji, na pia hutoa ushuhuda mahakamani. Wakati wanawake ama watoto wamebakwa, wanahakikisha waathirika wanapata kinga ya VVU ndani ya saa 72 na hutoa huduma ya ushauri kwa waathirika. Chris, ambaye ni mmoja wa wasaidizi aliyejitolea kutoka kwenye Parokia ya Palema alifanikiwa kutatua kesi ya msichana wa miaka mitatu aliyenajisiwa na babake mwaka wa 2011. Kwasasa babake anatumikia kufungo cha miaka kumi na mbili jela. Anasaidia pia kufungua mashtaka kwa mwalimu mmoja ambaye alimnajisi mwanafunzi wa miaka 14 na kwasasa mwalimu huyo yuko gereza akiingojia kuhukumiwa. Chris anahisi kwamba tangia mpango wa kujitolea wa GWED-G uanze, vita vya dhuluma vimepungua kwa kiwango kikubwa kwenye eneo hilo.

Uzito wa tatizo la dhuluma na kimapenzi na kijinsia kaskazini Uganda umetia shirikizo kwenye mfumo wa sheria ambayo tayari ni dhaifu. Maafisa wa polisi mara nyingi ni wahitimu wa shule za sekondari na hawana mafunzo kwenye masuala ya haki za kibinadamu wala hata kuhusiana na sheria, na kuna wanasheria wachache sana kwenye eneo hilo ambao huchukua kesi za namna hii. Shirika la Mtoto wa Vita wa Uganda limepata msaada wa fedha wa kufanya mafunzo kwa maofisa wa polisi, wahudumu wa afya, na wafanyikazi na mabaraza ya mitaa ili kujenga uwezo na kufanya upelelezi wa uhalifu na kukabiliana na waathirika. Wamefanya kazi pia na polisi ili kuhakikisha kila kituo cha polisi kina afisa mmoja mwanamke. Shirika la Mtoto wa Vita Uganda linachukua kesi zote kutoka eneo la kaskazini mwa Uganda, na huwarudisha nauli wateja wao wote ili waweze kuja na kupata ushauri wa kisheria. Pia wananasimamia huduma ya bure ya simu kwa waathirika wakike wa dhuluma.

Ingawa juhudi kama hizi hazizwezi kufuta machungu na misongo ya kimawazo uliyowakabili akinamama wa kaskazini mwa Uganda, wanaweza kuimarishwa na kuezeshwa wakianza jitihada kubwa za kujenga upya masha yao yaliyoharibiwa.

USAWA ||



ULEMAVU

Kote Afrika Mashariki watu wenye ulemavu wanakumbwa na ubaguzi kwenye kila ngazi. Kwenye familia, watoto huchukuliwa kama wasio na maana na hutengwa kutoka kwenye shughuli rahisi kama za kupika na kucheza; katika kupata huduma kama za elimu na afya, wanafamilia wengine ndio hupewa fursa ya kwenda shule na hupata matibabu ya bei ya juu, kwa kuwa wanaonekana kama walio na uwezo zaidi wa kufaulu; watu wenye ulemavu mara nyingi wanatengwa kutoka kwenye hafla za kijamii, zinazozihusu afya ama kilimo; na sera na sheria kwenye ukanda huu hazitilii maanani uwepo wa watu wenye ulemavu, wa mwili na hata ulemavu wa akili Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) pamoja na Jamii Wazi ya Mpango wa Haki kwa Walemavu wanasaidia mikakati ya vikundi vya haki ya walemavu kupata elimu.

ELIMU JUMUISHI NCHINI UGANDA

Nimepitia elimu jumuishi, ila kwa taabu nyingi sana, kwasababu ya vizuizi vya kimtazamo na umoja. Wakati mwingine singeweza kupata chakula cha mchana ama cha jioni kwasababu nilikosa mtu wa kunibeba mpaka kwenye chumba cha maakuli. Wakati mwingine nilishindwa kuingia maktabani, kwa hivyo niliwaomba marafiki zangu waende wosome kwa niaba yangu kisha wanipe muhtasari wa yale waliyosoma. Changamoto kubwa nilitambua kwa walimu hawakujua jinsi ya kukabiliana na ulemavu. Wakati mwingine mitihani ilifanyika kwenye madarasa ya maghorofani na wakati niliposaidiwa kupanda na mawazo hivyo singeweza kuwa makini kwenye mtihani. Somo la Kemia lilikuwa la lazima, ila sikuweza kukaa juu ya viti vile virefu kufanya majaribio

ya Kemia. Baadhi ya vikwazo hivi ndivyo vilinizorotesha ufanisi kwenye elimu yangu. Nilipomaliza shule, nilijua kwamba kuna wengi ambao walishindwa kupitia elimu jumuishi. Ndio maana nina hamu ya kujua ibara ya 24 ambayo inakuza elimu kupitia mtazamo wa haki na sio tu ukarimu.

Henry, Jukwaa la Maendeleo ya Vijana wenye Ulemavu

Jukwaa la Maendeleo ya Vijana wenye Ulemavu Uganda (YPDDF) wanatetea haki za vijana wenye ulemavu kikundi hiki kilianzishwa na vijana wenye ulemavu ambao walijumuika ili kujadili vikwazo hasi vya kimtazamo ndani ya jamii. Nchini Uganda, mara nyingi vijana na watoto wenye ulemavu wanadhaniwa kwamba wame logwa na wanaochukuliwa kwamba hawana tija kwenye jamii.

Ufanisi mkubwa wa YPDDF ni kuwa wameweza kubalisha mitazamo miongoni mwa walimu wakuu na wafanyikazi wa idara mbalimbali za elimu, ambao kwa sasa wanaamini kuna umuhimu wa kuwachanganya na kuwajumuisha watoto wenye ulemavu kwenye shule za kawaida. Ibara ya 24 ya Shirika la Umoja wa Kimataifa linaloshughulikia Haki za Watu wenye Ulemavu (UNCRPD) inakuza “elimu jumuishi”, ambayo inamaanisha kwamba watoto wenye ulemavu lazima wawe kwenye mazingira ya kishule kama watoto wale wasio na ulemavu, bila kuba-guliwa. Shule nyingine nchini Uganda kwa sasa wamefanya mabadiliko; na wamewapa mafunzo walimu ya jinsi ya kuwashughulikia watoto wenye ulemavu.

Matumizi ya redio na televisheni yamekuwa nyenzo kuu za kazi ya utetezi wa YPDDF. Wafanyakazi wa YPDDF wanakumbuka kisa cha familia moja ambayo mtoto wao alikuwa na ulemavu wa akili. Baada ya kumaliza shule ya msingi, mtoto huyo aliandikishwa kwenye shule ya sekondari na wazazi walikuwa washalipa karo. Ila, baada ya kuwasili shuleni, mtoto alinyimwa kuandikishwa baada ya mwalimu mkuu kugundua kwamba mtoto yule alikuwa na ulemavu wa kiakili. Baada ya kusikia kipindi cha YPDDF redioni, wazazi wa mtoto huyo walikwenda hadi kwe-

nye kituo cha redio. Mwakili wa YPDDF waliichukua kesi hiyo, ila walinyimwa fursa ya kukutana na yule mwalimu mkuu. Baadaye YPDDF walifanya maandamano ya amani nje ya shule hadi wiki tatu baadae mwalimu mkuu hatimaye akakubali kuwaona kutokana na mvuto mkubwa wa habari ulikuja baada ya maandamano hayo. Kwa wakati huu wazazi walikuwa washalazimika kutafuta shule nyingine kwa mtoto wao, ila mwalimu mkuu alikubali kurudishia familia hiyo karo yao pamoja na fidia, na kuhakikisha kwamba kamwe wasingenyima mtoto mwingine mwenye ulemavu uwezo wa kujitunga na shule yake.

Kikundi kingine cha utetezi ni kile cha Mkakati wa Vijana wenye Ulemavu nchini Uganda (AYDU), ambacho kimeanzisha mpango wa elimu unaohakikisha ushirikishwaji wa vijana wenye ulemavu kwenye taasisi za juu za elimu, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji. Mpango huu unalenga wanafunzi wenye ulemavu, watendaji wa elimu, na maafisa wa kitaaluma kwenye vyuo. Kupitia utetezi na ushirikiano na vyuo hivi, AYDU imefanikiwa kushuhudia vyuo vikuu vya Uganda vikianzisha na kutekeleza sera za ulemavu zinazoshughulika ubaguzi.

Kutokana na ushawishi wa AYDU, Chuo Kikuu cha Kyam-

bogo kwasasa kimesheheni wanafunzi ambao wanatumia viti gurudumu na basi ambalo husafirisha wanafunzi wenye ulemavu. Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Makerere kimenunua tarakilishi maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kuona, na maktaba mpya inakuja na mpango mpya ambao utahakikisha vitabu vya kusikiliza vinapatikana kwa wale wenye ulemavu wa kusikia. Wanafunzi wenye ulemavu wameanzisha vikundi mahiri chuoni ili kushirikisha viongozi wa chuo wahakikisha kwamba shida zao zinatatuliwa darasani na kwenye sehemu zao za makazi, na kuhakikisha lugha ya ishara inatumika ili kuwawezesha wasiosikia wajifunze pamoja na wenzao.

Harakati za haki za walemavu nchini Uganda zinasheherekea mafanikio waliopigana kwa nguvu kwenye nyanja za mageuzi ya sera. Mnamo Agosti 2012, Halmashauri ya Jiji la Kampala na Chuo Kikuu cha Makerere walishindwa na kesi iliyofunguliwa na Shirika la Harakati za Kisheria la watu wenye Ulemavu (LAPD). LAPD walifungua mashtaka kortini dhidi ya vyombo hivi viwili wakiwalazimu wazingatie Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2006) inayotoa agizo la majengo yote ya umma yawe na uwezo wa kutumika na watu wenye ulemavu. Katika hatua ny-

ingine, kufuatia mikutano mingi na vitisho vya mikakati ya kisheria na LAPD, Tume ya Mawasiliano Uganda (ambayo ni chombo cha udhibiti cha serikali) hatimaye kilitoa amri kwa vituo vyote vya televisheni vitumie mkalimani wa lugha ya ishara kwenye taarifa kuu za habari ama wafungiwe ndani ya mwezi mmoja. Na Machi 2012, Wizara ya Elimu ya Uganda ilipitisha Sera ya Mahitaji Muhimu na Elimu Jumuisi kubadilisha mwenendo wa kutawinyisha shule kwa walemavu. Kikundi kingine tulichokipatia fedha ni Jukwaa la Maendeleo ya Vijana wenye Ulemavu wa Kimwili (YPDDF). Kundi hili linafanya kazi na Kituo cha Mtaala, ambacho ni kitengo cha kisheria kilichopewa mamlaka ya kufanya marekebisho kwa mtaala wa mafunzo ya waalimu, kujumuisha muongozo wa jinsi ya kushughulikia watoto wenye ulemavu kwenye shule jumuishi. Maendeleo zaidi yanatarajiwa kwasababu Sheria ya Watu wenye Ulemavu (2006) kwasasa inatathminiwa kuioanisha na Shirika la Umoja wa Kimataifa linaloshughulikia Haki za Watu wenye Ulemavu (UNCRPD).

**WANAWAKE
WALEMAVU
'HUBAGULIWA
MARA MBILI'**

Wanawake nchini Uganda tayari wako katika hali mbaya kielimu kwani kuna dhana ya kitamaduni inayokataza wasichana kwenda shule. Nchini Uganda, ulemavu unahusishwa na laana, na wengine wanaamini kwamba walemavu walifanya makosa na ulemavu wao ni adhabu. Wanawake wenye ulemavu wanashindwa kupata ajira, kupata elimu na hutengwa na familia zao. LAPD wameweka mpango unaozingatia hususan upatikanaji wa haki wa wanawake wenye ulemavu. Utafiti uliofanywa na LAPD ulibaini kwamba wanaume ambao wana watoto na wanawake wenye ulemavu mara nyingi huwaacha kwasababu ya unyanyapaa. Kuolewa na kuwa na familia ni nguvu sana kwa wanawake wenye ulemavu kuliko wanaume wenye ulemavu kwasababu ya kirahi na dhana potofu ya kuwa wanawake walemavu hawawezi jifungua watoto.

Mimi ni mwanasheria, na nilienda chuo kikuu. Nilipitia changamoto nyingi. Kwanza kabisa singeweza kuingia kwa urahisi kwenye madarasa. Ningebebwa kama mzigo hadi kwenye madarasa ya ghorofa na hiyo ilikua kama adhabu kwangu. Niliomba darasa hilo lifundishwe kwenye ghorofa ya chini, ila ilikua ngumu sana kwani – mafunzo ya mwaka wa kwanza yalifanywa kwenye ghorofa ya

pili. Isitoshe pia kumbi za kufundisha na vyoo pia vilikua ngumu kutumia, na maisha chuoni yalikua magumu sana kwangu. Sijui nikuelezeje jinsi nilivyokabilia na vikwazo hivi ila ilikua ngumu sana kwangu. Wakati mwingine nilitoka kwenye kiti gurudumu changu na kupanda ngazi na wakati mwingine niliomba watu kama wanne wanibebe. Wakati mwingine nilihisi kwamba ninawasumbua wenzangu kwa kuwaomba wanibebe hivyo basi hukosa kuhudhuria mihadhara ili ni siwasumbue.


-Hope, Mkuu wa Kitengo cha Sheria cha LAPD

Mataifa ya Afrika Mashariki yametia sahihi na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (UNCRPD), na mashirika mengi kwenye ukanda huu yanafanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba haki hizi zinatimizwa kwa watu wote. Mkataba huu unazihitaji sheria zote kwenye mataifa wanachama kutathminiwa na kuainishwa kulingana na matakwa ya haki za kibinadamu. Mkataba huu umegeuza hadhi ya watu wenye ulemavu kutoka kwenye hali ya kuonewa huruma hadi kuwa watu walio na haki duniani kote. Kote kwenye ukanda huu, sheria zinatathminiwa upya kulingana na Mkataba huu, kwasababu kuu ya juhudi za watu wenye ulemavu wanadai haki zao.

KUSHEREHEKEA UTOFAUTI |



UBAGUZI WA KIKABILA NCHINI KENYA

 hini ya Sheria ya Usajili wa Watu, kila mwananchi wa Kenya anapaswa kujiandikisha na kuchukua kitambulisho cha kitaifa anapotimiza umri wa miaka 18 la sivyo atahukumiwa kisheria. Kwa Wakenya wengi huu ni mchakato waliozoea, ila Wakenya wenye asili ya Kinubi lazima wapi tie kwenye kamati ya ushahidi ambayo inajumuisha chifu wa mtaa, Afisa wa Tarafa, Shirika la Kitaifa la Ujasusi (NSIS), Kitengo cha Upelelezi wa Uhalifu (CID), na jopo la wazee wa mtaa, ambao wataamua iwapo watakubali maombi yao. Wanubi wengi wana haki ya kupata uraia wa Kenya chini ya Katiba, kwani wengi wao walizaliwa Kenya kama vile wazazi wao pamoja na mababu zao. Dhana ya kuwa Wanubi sio raia haeleweki na ni ya kibaguzi.

Wanubi sio jamii pekee inayopata shida hii ya ubaguzi katika kupata hati za utam-

bulisho. Wasomali, watu wenye asili ya Kiarabu ama Kiasia, na Wamakonde kutoka Msumbiji, pia wanahusishwa kwenye ushahidi huu ambao hufanya kwa njia za kiholela. Chanzo hiki huanza kupitia dhana kwamba wao sio raia kutokana na imani kwamba kabila lao ama rangi zao hazitambuliki. Jamii hizi wanatambua fika kwamba mchakato huu wa ushahidi uwe wa wazi zaidi na wenye msimamo mmoja.

Licha ya ishara muhimu wa kuwa na kitambulisho cha kitaifa ambacho ndicho kithibitisho cha uraia, vikwazo vinavyowekwa katika kupata hati hizi, zinawafanya jamii nzima kutoshiriki kikamilifu kwenye masuala ya kitaifa kama wakenya. Kitambulisho cha kitaifa ndio njia ya kupata haki zote ambazo Wakenya hupata kama vile ajira, elimu, haki ya kupiga kura, kufungua akaunti benki, kusafiri, kununua bidhaa pamoja na kuajiriwa kwenye

KUSHEREHEKEA UTOFAUTI I

idara ya polisi ama jeshini. Pia inasaidia kujikinga na usumbufu wa polisi na kukamatwa kiholela. Kwa kifupi, kitambulisho cha kitaifa ni ishara ya utaifa, na bila kuwa nacho, watu wanafanywa kuwa wasio na mataifa, jambo ambalo ni ukiukwaji wa sheria za kimataifa.

Kaskazini mwa Kenya pia wanasumbuka na suala la uraia, na jamii zinazoishi kwenye mpaka hususan wanadhaniwa kuwa wahamiaji haramu ama wakimbizi. Kulingana na ripoti iliyotolewa na Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KHRC) na iliyofadhiliwa na Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA), Foreigners at Home: The dilemma of citizenship in Northern Kenya (Wageni Nyumbani: Mtanziko wa uraia Kaskazini mwa Kenya), vizazi vya watu wa eneo la kaskazini mwa Kenya wanasaliwa popote wanapoishi nchini Kenya. Utafiti wa kimahojiano uliofanywa na KHRC ulibaini kwamba ni rahisi kwa watu waliozaliwa nje ya Kenya ambao wanatoka kwenye makabila makubwa kupata kitambulisho cha Kenya, zaidi ya wale wanatoka kwenye jamii zilizotengwa na waliozaliwa nchini Kenya.

“Nilizaliwa Wajir [kwenye mkoa wa Kaskazini Mashariki] kwa wazazi wenye asili wa Kenya. Nilienda kwenye shule

ya msingi huko Wajir na nika-jiunga na Starehe Boys Center, Nairobi. Nilitimiza miaka 18 nilipokua Starehe Boys Center. Timu ya maofisa kutoka kwenye Taasisi ya Kitaifa ya Usajili walikuja kuwasajili wanafunzi ambao walikua wamefikisha miaka 18. Kwa wanafunzi wote waliosajiliwa siku ile, ni mimi tu ambaye nilinyimwa usajili. Maofisi wa usajili walikubali kunisajili baada ya kupingana nao. Licha ya kuwa nilistahili kusajiliwa kama raia wa Kenya, nilisajiliwa tu kwasababu nilibishana nao.

Nina asili ya Kiluo. Nilizaliwa Dar es Salaam na nina cheti cha kuzaliwa cha Tanzania ambacho tulikipata Tanzania wakati wa kuzaliwa kwangu muda wazazi wangu walipoishi na kufanya kazi mwenye Shirika la Reli la Bandari ya Afrika Mashariki. Nilipata kitambulisho cha kitaifa bila bugtha yoyote kwakuwa nina asili ya Kiluo. Wakati nilipokuwa ninafanya maombi ya pasipoti ya Kenya, maofisa wa idara ya uhamiaji walikataa hati zangu kwasababu nilikuwa nina cheti cha kuzaliwa cha Tanzania. Nilisaka ushauri kutoka Sheria House jijini Nairobi kwajinsi ningepata cheti cha kuzaliwa na nikataarifiwa kuwa ningefaidika na usajili wa uzee wa kuzaliwa ambao nilipeleka maombi. Nilipata cheti cha kuzaliwa na baadaye nikaanza mchakato wa kupata pasipoti yangu.

Nina pasipoti ya Kenya, sio kwasababu nilizaliwa Kenya, ila kwa kua ni Mjaluo.”

(Wageni Nyumbani: Mtanziko wa Uraia Kaskazini mwa Kenya, uk. 35)

Kutengwa kwa wananchi wa kaskazini mwa Kenya pamoja na Wanubi, ulianza katika zama za kikoloni wakati watu walipogawanywa kama wananchi ama watumwa. Watumwa hawakutambulika kama raia, na ushiriki wao kwenye masuala ya umma yalikuwa finyu. Walitengwa kijamii na kiuchumi, na uwezo wao wa kupata huduma za elimu, hospitali, barabara, maji safi, ama huduma za kipolisi zilikuwa finyu, jambo lililowafanya jamii nzima kutengwa na kukosa maendeleo.

Ripoti ya KHRC, wageni nyumbani, ilivumbuliwa kwenye hafla iliyojumuisha mawaziri wa serikali, maofisa wa wilaya, pamoja na washikadau mbalimbali wa kaskazini mwa Kenya, na ikasababisha mwamko mpya kwa serikali kushughulikia masuala haya ya uraia kwenye katiba mpya ya Kenya.

OSIEA pamoja na Mradi wa Utawala, Ufuatiliaji na Utetezi wa Afrika (AfriMAP) walifanya uchambuzi wa kina wa nafasi ya uraia kwenye Katiba Mpya ya Kenya kwa niaba ya Tume ya Wataalamu wa Katiba, na

pia wakachapisha matokeo haya kwenye vyombo vya habari. Kwa kuwa sasa Katiba ya Kenya ya 2010 imepitishwa, OSIEA imekuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano na muungano wa asasi za kirai ujulikanao kama Chapter 3 (C3C) kushinikiza kutekeleza sheria ili kujumuisha sheria mpya za uraia pamoja na kufuatia maendeleo ya sheria zingine ambazo hazijapitishwa zinazohusu utaifa na uraia. OSIEA inawasaidia C3C kuimarisha ushiriki wa asasi za kiraia kwenye maendeleo ya kisheria za uraia, kufuatilia ubora wa sheria mpya na kuwa makini kwenye mwaada yote ambayo inangojwa kupitishwa kama sheria.

MIKAKATI YA KISHERIA

Nguvu-kazi ya Uraia Kenya, imepewa jukumu la kuandaa sheria mpya ya uraia ambayo inaendana na matakwa ya katiba mpya, na ambayo kwa umaalum inashughulikia kutokua na utaifa pamoja na masuala mengine. OSIEA imeshirikiana na Jamii Wazi ya Mpango wa Haki (OSJI) kufanya mkakati wa kisheria kama mbinu endelevu ya utetezi inayofanywa na washirika kadha wa kadha wa OSIEA kuishawishi nguvu-kazi hii kushigulikia ubaguzi unaowakumba jamii zilizotengwa nchini Kenya.

Katika hukumu ya kihistoria iliyotolewa Machi 25, 2011, Tume ya Afrika ya Wataalamu wa Haki na Maslahi ya Mtoto kwenye kesi ya *Watoto wa Kinubi v Kenya* ulieleza kwamba Kenya inakiuka haki za watoto wa Kinubi. Kwenye maswala ya ubaguzi, utaifa na kutokingwa kutokana na kutokua na utaifa/taifa. Kesi hii ilifunguliwa na watoto wa Kinubi kupitia wakali wao OSJI na Taasisi ya Haki za Kibinadamu na Maendeleo Afrika (IHRDA). Hii ndio mara ya kwanza tume hii imebaini kuwa taifa limekiuka haki za watoto, ambayo kwa kiasi kikubwa imefanikisha kilio cha Wanubi. Mkakati huu wa kisheria ni mhimili wa utetezi wa sheria ambao ulianzishwa mara baada ya kupitishwa katiba mpya.

Mnamo Januari 2011 Kikundi cha Waislamu Haki za Kibinadamu (MUHURI) ambacho kinafadhiliwa na OSIEA, walileta malalamiko, pamoja na Abdulhaleem Khalef El-Busaidy, dhidi ya utawala wa mtaa Mombasa, wakipinga matumuzi ya stakabadhi za serikali zilizovuja ambazo zinaagiza kwamba Waislamu wote, Waarabu na Waasia lazima watoe vyeti vya kuzaliwa vya mababu zao na vyeti vya dini kabla ya kupewa vitambulisho vya kitaifa. Mahakama Kuu ikifanya hukumu yake jijini Mombasa ilitambua kuwa

washtaki walikuwa na kesi halali na serikali ikashindwa kujitetea. Hukumu iliikataza Taasisi ya Kitaifa ya Usajili wa Watu kudai vyeti vya dini na vyeti vya kuzaliwa vya wazazi ama mababu kama kidhibiti-sho cha uraia. Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KNHRC), ambayo ni chombo cha kitaifa cha haki za kibinadamu, kwa ushirikiano na mashirika kadha wa kadha kutoka Kaskazini mwa Kenya walifungua kesi inayotaka iwekwe wazi kwamba mchakato wa usahili ni ubaguzi na ni kinyume na katiba. Kesi hii inaendelea.

Japo mengi yamefanywa, ushirikiano endelevu unaoimarisha jamii kujihusisha moja kwa moja na waunda sera unahitajika. Mafunzo yanapaswa kutolewa kwa wasaidizi wa kisheria (paralegal), hususan wale wanaotoka kwenye jamii ya Wanubi ili kujenga ufahamu wa hukumu hivyo kwa haki za Wanubi. Hatimaye, jamii ya Wanubi wanapaswa kupewa mafunzo ya kurekodi madhila haya ili kufichua tabia za unafiki wakati wa kutekeleza sheria hizi.

KUSHEREHEKEA UTOFAUTI II



KUJENGA UTAMBULISHO WA KITAIFA



namo Julai 2011 Sudan ya Kusini ilijitenga kutoka Sudan baada ya kura ya maoni ya kujipatia uhuru. Sudan ya Kusini iliibuka kutoka kwenye miongo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vinaaminika vililua watu karibu ya milioni mbili. Kwa miaka hiyo yote ya vita utambulisho mkuu wa Sudan ya Kusini ilielezwa kwa misingi ya upinzani kwa Sudan ya Kaskazini. Katika kipindi hiki cha baada ya uhuru, je Sudan ya Kusini inaweza kujenga utambulisho wa kitaifa ambao utahushisha utajiri wao wa makabila kadha wa kadha na kuachana na woga wa wageni? Je taifa hili jipya litahakikishaje kwamba wananchi wake wanahisi kama wamejumuishwa na

kuwakilishwa ilikuhakikisha usawa katika upatikanaji wa huduma za kimataifa, ajira na rasilimali kwa wananchi wake wote?

KUBADILISHANA UZOEFU KWENYE MASUALA YA UTAMBULISHO NA UJENZI WA TAIFA

"Ili serikali iwafanye watu wote wajihisi kama wananchi wa Sudan ya Kusini ni lazima waeleze kinagaubaga kwamba Sudan ya Kusini ni mali ya kila Msudan wa Kusini, na sio kwa kabila fulani, dini fulani ama kikundi fulani cha kisiasa. Kulitilia jambo hili maanani katika usambazaji wa rasilimali za kitaifa na katika masuala za kitawala, serikali imeeleza

waziwazi kwamba nchi nzima lazima ijishughulisha katika kutafuta, kuripoti, kuhifadhi, kuonyesha, kukuza na kusherehekea tamaduni ambazo ni kawaida kwa kila Msudan wa Kusini. Kulingana na ahadi ya sera hii, masuala ya kidini, sanaa, mifumo ya ndoa, lugha asili, mazingira asili, pamoja na maeneo ya kipekee ya ikolojia ambayo ni makao ya Wasudan wa Kusini lazima yashereheke kama mchanganyiko wa ishara inayowaleta pamoja watu wa Sudan ya Kusini.”

Dk. Jok Madut Jok, Katibu Msaidizi wa Wizara ya Utamaduni, Vijana na Michezo, Sudan ya Kusini

Mnamo Agosti 2012, Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) na Jamii ya Wazi ya Mpango wa Zaidi ya Mipaka ya Afrika Mashariki (EEBBP) walialika ugeni kutoka kwa watu binafsi kutoka kwenye mashirika ya kiraia, nyanja ya elimu na maofisa wa serikali kutoka Sudan ya Kusini kwa pamoja wafanye uakisi kwenye suala la ujenzi wa taifa pamoja na wenzao kutoka kwenye mataifa yaliyoibuka tu kama Slovenia, Macedonia, Eritrea, na Timor ya Mashariki. Mabadilishano haya yalileta muamko na umechochea mjadala wa umma kwenye suala hili la ujenzi wa taifa.

Vikundi vipya vimechipuka vikijadili jinsi ya kushughulikia kurudi na kujumuishwa kwa watu wanaorudi nchini baada ya vita pamoja na wakimbizi wa ndani, ikizingatiwa tofauti zao katika ufahamu na waledi. Shirika la Sauti kwa ajili ya Mabadiliko (Voice for Change) ni kikundi kinachoongozwa na aki namama, ambacho kilishiriki kongamano hilo kimeandaa midahalo ya jinsi kinamama wanaweza kuchangia katika kujumuishwa kwa Wasudan wa Kusini na kutoa mafunzo ya maadili yatakayo kuza umoja na uhimili wa kitaifa. Mpango wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi Sudan (SuDEMOP), ambao unafadhiliwa na OSIEA, wamezindua mpango wa kuzuia woga na chuki dhidi ya wageni kwa kuwalenga wafanyakazi wageni kutoka mataifa jirani kwenye miji na Sudan ya Kusini.

REDIO INALETA WATU PAMOJA

Nchi ya Sudan ya Kusini ina zaidi ya redio 97 za FM zilizoenea kote nchini. Redio ni muhimu sana Sudan ya Kusini kwani, kulingana na Wizara ya Elimu, asilimia 75 ya watu hawajui kusoma na kuandika. Kizazi kipya cha vijana “MaDJ” na watangazaji

wa vipindi vya maongezi, wamechipuka, ambao wanawasikilizaji wengi vijana wenzao na hujadiliana jinsi ya kuwaleta pamoja na kuwunganisha watu wa Sudan ya Kusini. OSIEA pamoja na Jamii Wazi ya Mpango wa Habari wanasaidia Mpango wa Amani wa Gurtong kuanzisha vipindi vya redio kwenye Redio Safari ya South Sudan ili kuwahabarisha watu kuhusu masuala ya utawala, maendeleo na makabila tofauti ya Sudan ya Kusini. Vipindi hivi vinarushwa kwa lugha ya Kiingereza na Ki-arabu cha Juba kwenye idhaa ya redio ikifikia majimbo manne kati ya kumi.

“LEO KUNA RAHA KUWA MSUDAN WA KUSINI”

Utajiri wa tamaduni za kimuziki, tamaduni za kishairi na sanaa nchini pia zimetoa fursa ya kujenga utambulisho wa kitaifa juumuishi. Katika mwaka wa 2012, Kampuni ya Sanaa ya Sudan ya Kusini (SSTC) waliandaa maigizo Sudan ya Kusini, Uingereza, na India ya mchezo wa Cymbeline wa Shakespeare, ambao maudhui yake ya vita na kisha kupata amani na umoja dhidi

ya mpinzani yanaambatana na historia ya nchi hiyo. SSTC inaundwa na makampuni mawili, moja wapo ni Kituo cha Kitamaduni cha Kwoto, ambacho kinafadhiliwa na OSIEA. Mchezo huo uligizwa kwa lugha ya Kiarabu cha Juba, mfumo wa Kiarabu kizungumzwacho Juba ambacho hakiandikwi na hutumika kama lugha ya mawasiliano na makabila kadhaa pamoja na Kiingereza. Mchezo huu wa kuigiza ulipata uwanda mkubwa wa matangazo ndani na nje ya nchi. Watayarishaji wote wawili wa mchezo huu wa Cymbeline wamesisitiza mchango wa utamaduni katika kujenga hali ya utambulisho wa kitaifa katika Sudan ya Kusini kwa kuleta pamoja makabila, kuinua hali ya utambulisho na kusaidia kutambua na kueleza nani ni Msudan wa Kusini wakati huu wa mabadiliko makubwa ya kisiasa wakati wa ujenzi mpya na utaiifa unaendelea.

"Hali ya furaha iliyotokana na mchezo huu wa kuigiza muiongoni mwa Wasudan wa Kusini waishio Ughaibuni unafanishwa tu na ule wa tamko la kuwa Sudan ya Kusini, kama taifa huru Julai 9 2011. Ilifuraisha kuona kwa mara ya kwanza, kwamba taswira hasi ya Sudan ya Kusini

ni kwenye vyombo vya habari kama mtoto anayekufa kwa njaa, ambaye hana nguvu na hata hawezi kufukuza nzi usoni pake, ikibadilishwa na waigizani wanaocheke kwenye mchezo wa 'Cymbeline' Mchezo huu wakuigiza pia umefanya Wasudan wa Kusini pia waanze kupinga dhana ya kushindwa: Misemo kama: "Sisi ni taifa jipya tunaanza kuanzia mwanzo" ama kielelezo "Roma haikujengwa kwa siku moja!". Inakaa nyepesi sana, ukilinganishwa na mafanikio ya sanaa ya Sudan ya Kusini ambayo miezi mine iliyopita, hata haikuwepo.

Wakati wa mapokezi ya kishujaa kwa waigizaji katika kituo cha Abbey, yaliyoandalwiwa na chama cha kinamama tarehe 5 Mei, Msemo uliorudiwa mara nyingi ilikuwa; "Leo kuna raha kuwa Msudan wa Kusini!" Hakuna ubishi kwamba utamaduni umeswalia kushinda kitu kingine chochote kuimarisha taswira nzuri ya Sudan ya Kusini kwenye ramani ya dunia kupitia mafanikio ya mchezo wa kuigiza wa 'Cymbeline'.

Mmoja wa Wasudan wa Kusini Ughaibuni Uingereza

UVUMBURI



AFYA NA HAKI



Mpango wa Afya na Haki na OSIEA umejengwa katika msingi wa ushirikishwaji wa watu wote-hata wale walio kwenye pembizo za kijamii kutokana na ubaguzi ama unyanyapaa. OSIEA, kwa ushirikiano wa karibu na Mpango wa Afya ya Umma (PHP), wanajitahidi kuhakikisha kwamba watu walio ukingoni, kama watu wanaoishi na magonjwa hatarishi kama vile VVU/UKIMWI, watumiaji wa dawa za kulevya, pamoja na wajane maskini wanaoishi na VVU wanapata huduma za afya.

OSIEA pia inashughulikia viashiria vya chini vya afya, kama vile uwezesaji wa kisheria na kiuchumi. Mpango huu unasaidia mipango isiyo ya kawaida, kama vile kuwafunza watumiaji wa dawa za kulevya kuwa wasaidizi wa sheria na kushirikisha haki za kibinadamu katika mipango ya kubalishisha tabia za mateja wa dawa za kulevya; kuhakikisha upatikanaji wa huduma

shufaa za matitabu pamoja na dawa ya morphine pamoja na kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa wanaoishi na magonjwa kama vile VVU na saratani; kampeni za kuhakikisha upatikanaji wa dawa bora na zenye bei nafuu kwa wote; na miradi inahusisha kujenga upya nyumba kwa wajane waliofurushwa majumbani mwao baada ya mabwana zao kufariki na VVU.

HUDUMA SHUFAA

“Huduma shufaa ni muhimu sana kwa wagonjwa wangu kwasababu magonjwa haya yanaweza kuwa yanauchungu sana. VVU inaweza kufika kiwango ambacho uchungu hauwezi vumilika pamoja na maumivu makali ya kichwa na uchungu kwenye viungo ambao hauwezi tibiwa na dawa kawaida za maumivu kama paracetamol, kwahivyo unahitaji dawa kali kama Morphine. TPCA walitufundisha jinsi ya kutoa huduma shufaa na matumizi ya morphine kupitia mdomo...Baadhi ya wagonjwa wengine tunajua

ubashiri wa magonjwa yao inakuwa miezi sita. Madaktari hawawezi tibu magonjwa haya hivyo basi wao hutibu tu uchungu.”

Daktari anayeshughulika na wagonjwa wanaoteseka na VVU, Kifua Kikuu na Saratani.

Mamia ya maelfu ya watu Afrika Mashariki wanaishi na VVU, wengi wao hawajui hali zao za Ukimwi. Hata utoaji wa damu za kurefusha maisha (ARVs), VVU mara nyingi huambatana na uchungu na viashiria vibaya kama vile maumivu ya utumbo, kichefuchefu na kutapika, vipele na kuharisha sana. Kwakuwa VVU inashambulia mfumo wa kinga, wengi hupata magonjwa kama Kifua Kikuu na Saratani ambazo huwa na athari mbadala za uchungu.

Huduma shufaa inapunguza maumivu sugu kwa wagonjwa mahututi, na kuwa kinga na uchungu usioepukika pamoja na kuwawezesha kufa kwa heshima. Serikali za Afrika Mashariki kwa taratibu wanaanza kuonyesha mwamko katika kujumuisha huduma shufaa kwenye sera na kuifanya moja wapo ya mwendelezo wa afya. Uangalizi unazingatiwa ili kupunguza maumivu na kuteseka kiholela na kupoteza heshima. Hii inajumuisha utoaji wa huduma za ushauri nasaha, maelekezo ya ki-roho, na wakati mwengine ushauri wa kisheria unahusi-

sha kuandika wosia na mipango ya urithi.

Katika wodi ya watoto katika Hospitali ya Nyerere jijini Dar es Salaam, Tanzania, zaidi ya watoto kumi na watano wanapumzika kwenye vitanda pamoja na mama zao ama wanacheza pamoja wakitumia magari ya kitoto na matofali ya kitoto. Kwa watoto wote hawa walio chini ya tiba ya saratani na resipi ya kemikali ya opioid ambayo imeangaliwa kwa uangalifu inawaepusha na kulazwa na kupiga kelele kila wakati kutokana na maumivu. Ule unafuu ambao watoto hupata unawezesha kucheza kama watoto wengine na wazazi hupata kitulizo cha akili. Kazi ya Chama cha Huduma Shufaa Tanzania (TPCA) pamoja na washirika wake kimesababisha mabadiliko kutoka kwa serikali, ambayo yameona kuboreshwa kwa huduma ya shufaa nchini, pamoja na miongozo mipya ya sera ya huduma shufaa. OSIEA ime-saidia TPCA kuongeza upatikanaji wa dawa ya morphine nchini. Kwenye vituo kadhaa vya matibabu, TPCA inatoa mafunzo kwa wahuduma wa afya na kuwafanya wahitimu katika kuiyeyusha kidonge cha morphine na inaweza kutumiwa na wagonjwa. Hapo awali dawa ya majimaji ya morphine ulipakana tu Dar es Salaam na ulisafirishwa hadi hospitali za mikoa, jambo lililosababisha ongezeko la bei.

KUPUNGUZA MAUMIVU

“Nilikuja Reachout mwaka wa 2003 wakati wa kipindi cha kunisaidia kuacha matumizi ya dawa za kulevywa za heroin. Kwasasa sijatumia kwa miaka tisa. Baada ya kumaliza mpango huo, nilikuja kufahamu kwamba Reachout walitaka kuanzisha mpango wa kuwafikia mateja na nilihimizwa kuwasaidia wenzangu ambao nao walikua wanajitahidi kuacha ulevi wa dawa za kulevywa kuwawezesha na kuwasaidia wajue hali ya VVU, kuwasaidia wapunguze matumizi wa dawa za kulevywa. Kama anatumia sindano ninamshauri jinsi ya kutumia kwa usalama halafu kuacha kujidunga na baada yake kuvuta na baadaye kuacha vyote kabisa.

Reachout ilinitambua na kunipa ujasiri wa kwenda mtaani na kupata mateja, na kuashauri kwa matibabu ya VVU. Wakati mateja wanajidunga sindano, tunawoonyesha jinsi ya kufanya hivyo salama. Tunatoa sindano safi na salama pamoja na usufi na tunawaambia wasibasibadilishane. Tunatoa elimu kwamba VVU inaweza kusambazwa kupitia hizo sindano. tangu niujiunge na Reachout nimewafikia mateja kama 3,000 hivi. Wengine wao wameacha kabisa matumizi ya dawa za kulevywa na wanaishi maisha mazuri, wen-

gine kwa sasa wana familia na wanaishi maisha yenye neema. Nimesaidia wenzangu kujua hali zao za VVU na kujua kwamba hata kama wameathirika sio mwisho wa maisha na kwa sasa wanaishi kwa matumaini na hawajihusishi na tabia hatarishi”

Mfanyikazi wa Outreach na teja aliyebadilika.

Monica, mama wa watoto wawili wa umri wa miaka 30 anayeishi Malindi Pwani ya Kenya amepambana na utumiaji wa heroin kwa zaidi ya mwongo umoja. “Uraibu wa dawa hizi ni kama kujaribu kufufua mwili wa mpendwa wako ndani yako, hisia za ukosefu wa matumaini na kukata tama pamoja na changamoto zote katika maisha-nafsi yangu ilikua imekufa”. Juhudi za kuwahimiza mateja kuacha moja kwa moja matumizi ya dawa za kulevya hazishighulikii kwa ukamilifu changamoto za uraibu. Kwa wale ambao hawawezi kuacha, ni muhimu kupunguza madhara ambayo wanapata, hususan maambukizi ya VVU.

Mbinu hii ya kupunguza maumivu humaanisha kupunguza madhara hatarishi ya dawa za kulevya kiafya, kijamii na kiuchumi kupitia mikakati ya kubadilishana sindano, utoaji wa huduma za kisheria na mipango ya kijamii ambayo hupunguza unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya



watumiaji wa dawa za kulevya kwenye jamii. Mipango hii huendeshwa pamoja na huduma za kurekebisha tabia za mateja. Haki za kibinadamu, pamoja na haki ya afya inajumuisha watu wote, hata watumiaji wa dawa za kulevya.

Hali ya utumiaji wa dawa za kulevya Malindi inashangaza kwani jamii hii kwa kiasi kikubwa ni ya kiislamu, na watumiaji wengi ni wanawake. Watumiaji wa dawa za kulevya nchini Kenya wananyanyapaliwa, hususan wanawake, ikiwaacha watumiaji wengi wakikabiliana na uraibu huo kwa usiri na aibu. OSIEA kwa ushirikiano na Mradi wa Omari unajitahidi kubadilisha haya. Watumiaji wa dawa za kulevya wanaopata nafuu wanafudnishwa kuwa wasimamizi wa sheria (paralegal) na wanaenda maeneo ya maskani mbaya, na wanaongea na watu kuhusu jinsi watakavyopata huduma za afya, na kuhusu haki zao watakapo patikana na umiliki wa dawa za kulevya. Wasaidizi hawa kisheria wanaungwa mkono na wanasheria wasiotoza huduma zao na husimamia ushauri wa kisheria wanaopatiwa, na uhakikisha kwamba wale wanaopatikana na umiliki wa idadi ndogo ya mihadarati hawapati mashata ya usafirishaji wa dawa za kulevya ambayo huja na kifungo cha gerezani.

Kituo cha Reachout ambacho kipo hapo karibu kwenye mji wa Mombasa pia hutoa huduma za kupunguza maumivu kwa wanaotumia dawa za kulevya. Mradi huu ulipoanza mwaka wa 2003, jamii ya kihafidhina ya Mombasa Old Town ilikua wakali sana kwa watu wa eneo hili ambao walikua wanatumia mihadarati; lakini kwa taarifa, maarifa na mawasiliano, watu walibadilika. Reachout inawasaidia watu kuelewa kwamba kuna huduma za matibabu zinazopatikana na sio jukumu la shirika hilo, bali jukumu la jamii, na hii inajumuisha polisi, chifu, na wazee wa kijiji.

Wasaidizi wa sheria wali-ofunzwa na Reachout wanafanya kazi na idara za marekisho kama vile magereza, huduma za majaribio na vituo vitano vya mapolisi mjini Mombasa. Wanasaidia watu waliokamatwa na tuhuma za dawa za kulevya kushughulika kesi zao kwa haraka kupitia mahakama na kuhakikisha kwamba hazicheleweshi katika uamuzi. Hivyo hivyo, MUHURI imekuwa ikifanya kazi na wafungwa kwenye masuala ya haki tangu mwaka 2006. Nchini Kenya kuna ulimbikimbizi mkubwa wa kesi na inaweza kuchukua hadi miaka tisa kati ya kukamatwa na kuhukumiwa. Idadi kubwa ya kesi MUHURI inayoshughulikana nazo ni zile zinahusiana na matumizi wa dawa za kulevya, ama

zinahusiana na 'ulanguzi' na karibia asilimia 60 ya kesi kwenye daftari la usaidizi la MUHURI zinahusiana na mihadarati, ambayo ni idadi kubwa, ikizingatiwa kwa kila siku wanashughulikia kesi 15 hadi 25.

MIPANGO YA KUPAMBANA NA BIDHAA BANDIA NA UPATIKANAJI WA DAWA

Kwenye ukanda wa Afrika Mashariki, kama asilimia 80 ya watu wanaishi vijijini, na zaidi ya asilimia 30 wanaishi chini ya mstari wa umaskini, jambo linalofanya wategemee huduma ya afya ya umma.

Dawa katika ukanda huu ni kama mara tatu au nne ghali zaidi ukilinganisha na viwango vya kimataifa, na ughafi wake unaweza kuwa kati ya asilimia 25 na asili mia 500. Bila dawa nafuu mara nyingi watu huishi kunywa dozi nusu za dawa, jambo ambalo huihua usugu wa dawa kwenye magonjwa kama Kifua Kikuu.

Muungano wa Kukuza Afya na Maendeleo ya Jamii Uganda (HEPS Uganda) inasaidia AFYA Club 5000 ambayo ina wanachama 850 ya watu wanaishi ya VVU huko Wakiso, mji uliopo takriban kilometa 15 kutoka kwenye bohari kuu la dawa la serikali

mjini Entebbe. Wanachama wa klabu hii wanayo matazizo megii katika upatikanaji wa dawa. Neriah ni mkuugenzi wa klabu hiyo, na kwa kuwa yeye pia anaishi na VVU anaelewa umuhimu wa upatikanaji wa mara kwa mara wa dawa zake za kurefusha maisha (ARVS).

“Wakati wagonjwa wa VVU hawawezi kupata dawa zao za muhimu, wanachoka na kuacha kabisa mfumo mzima wa kumeza dawa, jambo ambalo huwafanya wawe sugu wa dawa na hufa kiholela. Endapo unasitisha kwa muda matumizi ya dawa, unaanza kusikia kama unaumwa tena baada ya mwezi mmoja ama miwili, halafu unadhoofika na kuanza kupata maambukizi. Ni kama kupigana katika vita na jeshi ambalo linarejea nyuma, lakini linarudi na nguvu kali na kukupiga kwa nguvu zaidi. Mara tunapokua sugu wa dawa rahisi tunahitaji dawa zenye nguvu na ghali zaidi. Kati ya mwaka 2009 na 2011 wanachama wetu watano walifariki kutokana na kuwa sugu wa dawa. Watu wanapoteza matumaini na hawajui hata watapata wapi dawa za kurefusha maisha (ARVs) kwa minajili ya kupunguza usugu. Wanapata magonjwa nyemelezi kama malaria na hawamudu gharama kununua dawa hivyo wanakufa”

-Neriah, Mkuugenzi wa AFYA 5000 Club, Uganda

HEPS inawasaidia watu kama Neriah kuwa wakufunzi miongoni mwa watu wenye rika lao na ambao wanaweza kuwasaidia watu kuelewa umuhimu wa uzingatiaji wa dawa na kuhamasisha jamii kudai haki zao za kupata dawa muhimu.

Mara nyingi mtu akijaribu kununua dawa kwenye duka la dawa anakuta kuna upungufu wa dawa. Ukosefu wa dawa, kama zijulikanavyo, ni matukio la kawaida kwenye vituo vya afya kijijini ambavyo huishiwa na dawa kwa vipindi virefu, na kuwalazimisha wagonjwa kununua dawa zao kwenye sekta binafsi ambapo gharamu zipo juu na mara nyingi huwa sio za bei nafuu.

OSIEA inaazimia kukuza upatikanaji kwa urahisi wa dawa muhimu na kwa bei nafuu. Mwanzoni mwa mwaka 2009 kampeni ya “komesha ukosefu wa dawa” ulizunduliwa kama mpango wa Hatua ya Kimataifa ya Afya (HAI), Oxfam, pamoja na washiriki kadhaa wa Kiafrika kwa msaada wa OSIEA na PHP. Kote Afrika Mashariki, mkakati huu wa kampeni uliimarisha mashirika ya kiraia. HAI Afrika inasaidia mafunzo kabambe ya vyombo vya habari ili kuongeza uelewa ilikuvingiza haya masuala kwenye vyombo vya habari nchini, na kuifanya serikali kuanza kuzungumza maswala ya upatikanaji wa dawa.

Katika mwaka wa kwanza wa kampeni, serikali ya Uganda ilitilia maanani malalamishi kwa kulainisha mfumo wa kuagiza dawa. Hifadhi ya Taifa ya Dawa (NMS) uliongezewa fedha na uhuru wa kujiendelesha, rais na wanasiasa walijitokeza wazi kushitimu upungufu huo, na ofisi ya Rais uliunda sehemu ya kufuatilia dawa. Mabadiliko katika sera na utekelezaji katika wizara ya afya na NMS tangia mwaka 2009, imeongeza kwa kiwango kikubwa uwepo wa dawa muhimu kwenye sekta ya umma. Serikali kwa sasa imeweka mfumo mpya wa usambazaji ili kushughulikia upungufu kwenye vituo vya afya na ulimbikizi wa dawa kwenye vituo vingine.

Nchini Kenya msisitizo ulikuwa kwenye ushawishi wa uandaaji wa bajeti. Muungano wa asasi za kusahaidia waliandaa mikutano na mawaziri wa serikali na wakafanikiwa kushawishi ongezeko la fedha kwenye dawa muhimu kwenye makadirio ya bajeti, na kwa sasa Kenya ina bajeti maalum ya dawa muhimu. Vyombo vya habari vya Kenya vilipiga picha rafu za dawa za Shirika la Usambazaji wa dawa la Kenya (KEMSA) ambazo zilikuwa zimeachwa kwa muda mrefu na zilikuwa zimeharibika, ikizingatiwa kwamba maduka ya dawa nchini yalikuwa yamepungikiwa na

dawa hizo na yalikuwa yanan-gojea akiba mpya. Kuto-kana na kampeni hii KEMSA kwasasa imejiimarisha upya, hata kama changamoto zimebakia.

Tatizo la upatikanaji wa dawa limezidishwa na kupitishwa kwa sheria kote Afrika Mashariki ikipambana na dawa bandia, ila kwa udhairsi halisi kukaza utekelezaji wa haki miliki kama hatua ya kupiga marufuku dawa mwigo. Tatizo la dawa duni halitasuluhishwa kwa kupanua matumizi ya haki miliki ili kuezeka vizuizi vya biashara kwaajili ya dawa mwigo. Badala yake, mashirika ya kudhibiti lazima yaimarishwe ili kufanikisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa kwenye soko.

Katika hukumu kihistoria nchini Kenya Aprili 20, 2012 iliamuliwa kwamba baadhi ya vifungu vya Sheria ya dhidi ya Bidhaa Bandia ya mwaka 2008 havitahusisha dawa mwigo-jambo ambalo litalinda upatikanaji wa matibabau ya siyo ya gharama. Kesi hii ilifunguliwa na watu watatu wanaoishi na VVU, kwa usaidizi wa wafadhiliwa wa OSIEA kama vile Muungano wa Kenya wa Masuala ya Sheria na Maadili ya VVU na UKIMWI (KELIN) na HAI Afrika, na wakahoji sehemu mbali mbali ya sheria hiyo dhidi ya bidhaa bandia ya mwaka 2008 ambayo ili-changanya kizuizi wa bidhaa

bandia na ukiukwaji wa haki miliki, hivyo kutishia uagizaji kutoka nje wa dawa mwigo, pamoja na dawa za kurefusha maisha (ARVs) kwa watu wanaoishi na VVU. Hukumu ilieleza kwamba ulinzi wa haki miliki kwa bidhaa hauwezi kuzidi haki ya kuishi, haki ya afya na haki ya utu ambazo zimeainishwa kwenye katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Wanaoshika haki miliki za bidhaa kwa hivyo hawawezi kutumia sheria hii kuhalalisha uzuizi wa uagizaji kutoka nje wa dawa mwigo, kama ulivyo-oadhaniwa na waliofunguwa mashataka.

Mswaada kama huu uliletwa mbele ya bunge la Uganda, na HEPS-Uganda pamoja na Kituo cha Haki ya Binadamu na Maendeleo (CEHORD) wamefanya kazi kwa karibu na mawaziri kuhakikisha mswaada huu hauhatarishi upatikanaji wa dawa mwigo.

Nchini Kenya na Uganda mfuko wa rasilimali wa serikali bado ni mdogo katika utoaji wa dawa za kutosha, kuwa na miondombinu fanisi na nguvu-kazi ambazo zitaweza kutimiza matakwa ya umma na kuhakikisha huduma toshelezi ya afya. Kwa hivo hatua mbadala katika uchangiaji wa fedha kwenye huduma ya afya kama lengo la upatikanaji wa huduma bora za afya duniani litatimizwa. La zaidi pia, kuna haja ya kuongeza uamasishaji wa

jamii ili umma uelewe haki zao ili kuwaajibisha wale waliokuwa madarakani, pia kuelewa wajibu wao katika kuboresha afya majumbani na kukosa tabia bora za kiafya.

UPATIKANAJI WA HAKI NA AFYA

Kwa wanawake wengi wanaoishi Afrika Mashariki VVU sio tu tatizo la kiafya. Hata kama wanawake wana haki za kisheria kumuliki na kurithi mali, kitamaduni, hali hizi hazitambuliki, hususan kwenye jamii za kijijini. Hii inamaanisha kwamba mabwana za hawa wanawake wanapofariki na VVU, wanalaumiwa kwa ugonjwa ule na kufukuzwa kutoka kwenye boma zao na familia ya mume pamoja na kunyang'anywa mashamba, jambo ambalo huwaacha wanawake hawa bila makazi na umaskini. Hii huwafanya wanawake hawa wajikute katika hatari nyingine kutokana na umaskini na watahitaji kujitafutia kwa jinsi yoyote ile, hujumuisha pia umalaya. Kwa wanawake wanaoishi na VVU tayari wanajihatarisha na maambukizi mengine, na inakuwa vigumu kubaki katika matibabu bila lishe toshelezi ama ya mara kwa mara na makazi yaliyo salama. Wanawake kidogo wanauwezo wa kwenda mahakamani. Mara nyingi huwageukia wazee wa jadi kwenye jamii


kwa usaidizi. Muungano wa Kenya wa Masuala ya Sheria na Maadili ya VVU na UKIMWI (KELIN) wameshirikiana na mabaraza ya wazee wa kitamaduni huko Nyanza ambao husuluhisha kesi za kunyimwa na kupokonywa urithi kwa kutumia njia za kitamaduni katika kusuluhisha mizozo. Chini ya kifungu cha 159 cha Katiba ya Kenya, mfumo wa kitamaduni ya kusuluhisha mizozo inakubalika iwapo tu haikinzani na sheria ya haki za kibinadamu. KELIN ilianza mradi wa miundo wa kitamaduni pamoja na majukwaa ya midahalo kwenye jamii na kuhusisha majane, wazee, na maofisa wa serikali, ili kuhakikisha jamii wanaelewa. Hii ilifuatiliwa na mafunzo ya haki za kibinadamu na ya kisheria kwa wazee ili kuhakikisha wanatoa ushauri ambao ni wa haki na wakisheria.

“Njia hii ya kitamaduni inafanisi sana kwani inaleta mahusiano mazuri kwenye familia kwa kuwa ni ya kirafiki na inaleta majadiliano na hakuna ambaye ni mshukiwa, hakuna mtuhumiwa, tunapatana na kujadili kuwa tunatofauti kati ya watu wanaoishi nasi kwa hivo watu hupata kuelewa haki zao kwenye jamii. Mara wanapokuja kuelewa hili wanafurahi sana na kila mmoja anakubalika ila ukiwapeleka mahakamani kuna kuwepo uadui mwingi. Kwa matumizi wa mbinu zetu za kitamaduni

tunakuza mapendo na urafiki. Na pia inachukua muda mfupi wakati tunasuluhisha kesi za namna hii ila zikipelekiwa mahakamani unafahamu jinsi zinazungushwa na jambo moja linaweza kuchukua muda mrefu sana.”

-Kasuku Kalolo, Mzee kwenye Baraza la Wazee la Wajaluo

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita KELIN wamejihusisha na kesi 114 zinazohusu kunyimwa na kupokonywa kwa urithi. Mapema mwaka 2012, Baraza la Wazee la Wajaluo ilitoa uhukumu kwenye kesi za wanawake 70, ambao waliweza kurejea majumbani mwao. Wanawake wengi waliosaidiwa na mradi wa muundo wa kitamaduni wanakuta kwamba baada ya kushinda katika haki zao walizonyimwa, nyumba zao huwa zimebomolewa kinyemela na familia za bwana, ama kipande cha ardhi walichorithiwa kimenyakuliwa kwa wale wanawake wanayonge kabisa KELIN huwapa msaaada wa vifaa vya ujenzi ili waweze kujenga nyumba ya kawaida ya kuishi kwenye shamba lao. Wanajamii wanahusishwa kuwasaidia wajane kujenga nyumba, jambo ambalo huimarisha uhusiano kati ya mjane na jamii, na wajibu nao kwa mjane kama mmoja wa mwanajamii.



UADILIFU



UPATIKANAJI WA TAARIFA KWA UMMA

Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) inafanya kazi na washiriki nchini Kenya, Uganda, Tanzania na Sudan ya Kusini kutetea utungwaji na utekelezaji wa upatikanaji wa sheria za taarifa ili kuwafanya wananchi wakawaida kufahamu maamuzi ya serikali ambayo yanagusa maisha yao. Sehemu ambapo imechewa katika kujibu madai haya, washirika wa OSIEA wametafuta mbinu mbadala kama vile kujenga ujuzi wa ufuatiliaji wa jamii, utetezi na mikakati ya sheria inayosukumwa na wanadamu ambayo imeazimia kuilazimisha serikali kuweka wazi baadhi ya taarifa fulani.

USALAMA WA KITAIFA

Usalama wa kitaifa ni moja ya sehemu ambayo, kwa hali inayoeleweka, ni ngumu kupata taarifa. Hata hivyo, dhana hii ya usalama wa kitaifa inatumika kwa namna pana ya kuficha ufiisadi, utesaji na matumizi ya madaraka. Mnamo mwaka 2012, mashauriano ya kikanda yalileta pamoja wawakilishi kutoka kwenye wizara mbalimbali za Afrika Mashariki, polisi na mashirika ya kiusalama na mashirika ya kiraia kutoka kote Afrika Mashariki kujadili na kutoa mapendekezo kwenye Rasimu ya Kanuni ya Usalama wa Kimataifa na Haki

ya kupata Taarifa. Kanuni hizo zina lengo la kutoa mwongozo kwa waandaji wa sheria wanaojihusisha katika marekebisho ama kutafsiriwa kwa sheria zinazolinda uwezo wa serikali kuzuia taarifa ama kutoa adhabu kwa wachapishaji wa taarifa kwa misingi ya usalama wa kitaifa.

Rasimu hii ni matokeo ya mashauriano ya kina baina ya wataalumu wa kimataifa, mashirika ya kiraia, vituo vya elimu na wasimamizi wanne wa Umoja wa Mataifa na wengine wa ukanda huu wa masuala ya uhuru wa kujitendeleza. Mkutano huu ulikuwa mpango jumuishi wa OSIEA pamoja na washirika wengine ya Jamii ya Wazi (OSJI) na Mfuko wa Haki ya Kupata Taarifa. Siku mbili za majadiliano changamfu ilizalisha maoni yenye thamani kutoka kwenye muktadha wa Afrika Mashariki ambayo yatajumuishwa kwenye toleo la mwisho la kanuni hizo.

Katiba mpya ya Kenya imeleta haki mpya zinazohusu taarifa, uhuru wa vyombo vya habari na utekelezaji wa haki. Katiba hii ya mwaka 2010 pia inaeleza kwamba usalama wa kitaifa sio nyanja ya kipekee ya jeshi. Ila bado upatikanaji wa taarifa bado ni ngumu hususan katika operesheni za

kuzuia ugaidi zifanywazo na mashirika ya kiusalama ya Kenya ambayo hutumia njia zisizohalali kukabidhiwa washukiwa wa Uganda, kukamatwa kiholela na kuwawa kiholela. OSIEA iliunga mkono kesi kwenye Mahakama Kuu ya Kenya hadi Uganda kusimama mbele ya Mahakama kwa tuhuma za kulipua bomu Kampala mwaka 2010. Wanaume wote watatu walikamatwa Kenya bila kuwekwa katika mifumo ya kisheria ya kukabidhiwa kwa washukiwa kutoka nchi moja hadi nyingine na kuchukuliwa na magari ya polisi na kukabidhiwa kwa dola ya Uganda. Mahakama Kuu walitoa hukumu kwamba kukabidhiwa huko hakukuwa halali, ila Mahakama hawakuweza kuendelea zaidi kwa kuwa wanaume hao walikuwa nje ya mamlaka yao nchini Uganda. Baada ya kufeli katika majaribio kadhaa ya kupata uwajibikaji kwa kuiomba serikali ya Kenya kuweka wazi ni nani aliyetoa maamuzi ya kuwazuia na kuwasafirisha wale washukiwa wa ugaidi Uganda, kesi ilifunguliwa kwenye Mahakama ya Kikatiba ambapo serikali ilikiri kutenda hicho, ila walikataa kutoa majibu ya ombi la uhuru wa taarifa kwa misingi ya usalama wa kitaifa.

UTETEZI KWAJILI YA SHERIA

Nchini Sudan ya Kusini, miswaada miwili ya sheria imeidhinishwa na serikali na inapelekwa mbele ya bunge kwajili ya kupitishwa kama sheria. Miaka ishirini ya vita nchini Sudan imeacha urithi wa udhibiti wa vyombo vya habari. Wakati wa vita, vyombo vya habari vilitumika kama dhana ya propaganda, na wazo zima la taarifa kama chombo cha huduma kwa umma lilipotea. Kwa sasa, changamoto ni kubadilisha mawazo hayo na vyombo vya habari lazima vijichunge vizuri vinaporipoti masuala kuhusiana na usalama wa kitaifa. Umma una haki ya taarifa iwapo tu haitahusiana na usalama wa kitaifa, ila mahakama haina mamlaka juu ya masuala yanayohusiana na usalama wa kitaifa, hivyo taarifa inaweza kuainishwa kiholela tu. OSIEA inafanya kazi na Chama cha Maendeleo ya Vyombo vya Habari Sudan ya Kusini (AMDISS) kufanya utetezi wa kupitishwa kwa sheria za vyombo vya habari ambazo zinaendana na viwango vya sheria za haki za kibinadamu za kimataifa.



Nchini Tanzania, Ofisi ya Taarifa kwa Wananchi (TCIB), ambayo inafadhiliwa na OSIEA, inajihusisha kikamilifu katika muungano wa kitaifa kuimarisha na kujadili upatikanaji wa sheria ya taarifa, mingairi ya uskilivu mdogo kutoka kwa serikali. Mwaka 2007, serikali iliandaa mswaada wa utata wa uhuru wa vyombo vya habari ambao ulianzisha mfumo wa kusajili wanahabari wote na vyombo vya habari pamoja na ofisi ya kuangalia viwango katika sekta hio. Mpango huo haukuwapendekeza vyombo vya habari na washika dau wengine wa haki za binadamu ambao walihisi kwamba ni mbinu ya serikali iliyoazimia kuondokana na uhuru wa vyombo vya habari. Washikadau wa vyombo vya habari walitoa mapendekezo ya kufanya marekebisho kwenye mswaada huo, pamoja na mapendekezo ya kukataza maofisa kwenye sekta ya umma na binafsi kutoa taarifa kwa umma pamoja mifumo wazi na mfumo wazi panuzi ambao utaipatia kila mwanadamu fursa wazi ya kudai taarifa za umma. Serikali iliichomoa mswaada huo tata, ila tangu siku hiyo hawajaonyesha haja ya kuandaa mswaada mpya wenye marekebisho.

UTEKELEZAJI WA SHERIA

Hata pale ambapo kuna-patikana sheria ya taarifa, utekelezaji bado unabaki changamoto. Uganda ni mojawepo ya nchi chache Afrika ambazo zina sheria ya uhuru wa taarifa, ila ili-chikua miaka kadhaa kabla ya kanuni za utekelezaji zilitolewa. Licha ya sheria hii, uelewa wa umma kwenye masuala nyeti, kama vile sera za mafuta ama usalama mara nyingi huzuiwa na serikali kwa kutumia mikakati ya kisheria kudai taarifa zitolewe kwa umma. Kumekuwa mikakati ya kisheria kudai taarifa zisitolewe kwa umma, kumekuwa na mafanikio kiasi nchini Uganda. Moja kati ya jitihada hizi ni usaidizi uliotolewa na OSIEA kusaidia Mpango wa Hifadhi wa Rasilimali za Kihistoria (HRCI). Wakati serikali ya Uganda ilipotangaza lengo lake la kubomoa makazi yenye umri ya miaka 100 ili kujenga kituo binafsi cha biashara cha ghorofa 60, HRCI walifungua kesi ili kuilazimisha Wizara ya Utalii kutoa stakabadhi kama stakabadhi halisi ya umiliki wa eneo, utathmini wa athari ya mazingira, tath-

mini ya turathi za kitaifa, na makubaliano ya zabuni. Kutoa taarifa kwa stakabadhi hizi ingedhihirisha wazi ukiukwaji wa sheria katika mpango huu. Kufuatia taarifa hizi kutolewa, Wizara ya Utalii walitangaza Julai kwamba wanasitisha mpango huu.

Muungano wa Mawakili wa Maendeleo na Mazingira (ACODE), ambao ni muungano huru wa kujadili masuala ya sera za umma kuhusu utetezi wao ambao unahusu sheria na mfumo wa kwamba baraza la mawaziri hufanya maamuzi bila kuhusisha jamii zinazoathirika na utafutaji wa mafuta kwenye maeneo yao. Wakati utathmini wa athari ya mazingira unafanywa, jamii hizo hazipewi fursa kushiriki kikamilifu, hata kama majadiliano ya wazi yanatambulika katika kanuni. ACODE pia walibaini kuwa watu hufurushwa mara kwa mara bila ya kupewa fidia na serikali ama makampuni yanayofanya utafiti wa mafuta, jambo ambalo linakiuka haki za katiba za watu hawa. ACODE wanahoji ni kwanini serikali imeficha mikataba ya ugavi ya uzalishaji, wakati umma una haki za kisheria za kushirikishwa kama moja wapo

ya makubaliano kwenye mikataba hii, na pia bunge lazima litoe uangalizi jambo ambalo halipo. ACODE walifanikiwa kupata hakikisho kutoka kwa serikali wakati wa mkutano wao na wana-chama, kuandaa mkakati wa kimawasiliano ambao utajumuisha umma. ACODE wanaratibu mikutano ya kila mwezi ya mashirika ya kijamii ya kubadilishana taarifa, na wameanzisha tovuti ya muungano wa mashirika ya kisheria yanayohusiana na mafuta na gesi nchini Uganda. Muungano huu umekuwa wa nguvu, na wakati rasimu ya awali ya Msawaada wa Mafuta ulipoandaliwa, wizara iliwapo muungano huu na kuomba mapendekezo yao, ambayo ilikuwa hatua kubwa mbele. Pia nchini Uganda, OSIEA inasaidia GreenWatch ambayo inafanya kazi na jamii zilizopo kwenye maeneo ambayo mafuta yanapatikana kufutilia athari za mafuta kwenye mazingira. GreenWatch walifungua kesi mwaka 2008 ikiomba kuwalazimu serikali kuweka wazi yaliyomo kwenye mikataba ya ugavi ya uzalishaji chini ya Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa. Hata hivyo, kesi hii imepeleka mbele mara nyingi sasa.

KUKUZA UWAZI KWENYE MAENDELEO YA MIUNDOMBINU YA UMMA

Mwaka 2003, serikali ya Kenya ilianzisha Mfuko wa Maendeleo wa Majimbo (CDF), na kuwapa kila mmoja wapo wa wabunge 2010 takriban dola milioni moja kila mwaka kwajili ya maendeleo ya jamii. Waliweza kutumia fedha hizi bila uangalizi wa chombo huru. MUHURI walihamasisha wananchi wa kawaida kuingilia kati na kutoa uangalizi, kwenye eneo bunge la Likoni mjini Mombasa, kupitia ukaguzi wa kijamii. MUHURI walitoa mafunzo kwa wanaharakati wa kijamii kukusanya rekodi kutoka kwenye ofisi za serikali za CDF, kukagua maeneo ya miradi ya CDF, na kuleta taarifa hizo walizopata mbele ya umma. Jamii hiyo ilifanikiwa kwenda kwenye ofisi zao za CDF kudai taarifa kuhusiana na matumizi ya fedha za CDF kwenye maeneo yao, na kukagua rekodi za matumizi ya fedha ambazo huonyesha kwa kina ni kiasi gani cha fedha zilitumika kwenye kila mradi. Timu hiyo ilienda kwenye shule ya msingi ambayo ilijengwa

kutumia fedha za CDF. Wali-chukua vipimo halisi vya jengo hilo na kulinganisha kila kitu na rekodi za Mswaada wa Viwango. Rekodi zilionyesha kwamba madirisha kumi na mbili yalilipiwa, ilhali kwa ukweli yalikuwa 8 peke yake; kuna malipo ya milango 2 ilhali kulikuwa na mlango mmoja uliojengwa na kuta moja tu iliyopigwa rangi. Kwenye kijiji kingine, Shule ya Sekondari ya Mrima ambayo rekodi inaonyesha iligharimu milioni 4.8 za Kenya ya fedha za CDF hai-kuwepo. MUHURI ilihamasisha jamii nzima, pamoja na wanaume, wakinamama na watoto, kuja mbele ya hadhara kukutana na viongozi wa serikali ambao wanahusika na fedha za CDF; ili kuwawajibisha kuhusiana na upotevu wa fedha hizo. Mara baada ya ukaguzi wa fedha wa ujenzi wa shule ya Likoni, MUHURI walifungua kesi mahakamani kuhoji sheria ya CDF kikatiba. Wanaharakati kutoka Likoni pamoja na majimbo mengine saba waliandaa ukaguzi wa kijamii wa fedha za CDF waliungana kuanzisha kampeni ya kitaifa wakikabiliwa na la-wama nyingi, Juni 2009, serikali ya Kenya iliunda jopo-kazi ya kutathmini kwa kina sheria ya CDF na baadaye ikabanduliwa.

MSHIKAMANO & UMOJA KAZINI



KUWAKINGA WATETEZI WA HAKI ZA KIBINADAMU

Watetezi wa haki za kibinadamu katika ukanda

huu mara kwa mara wanakumbwa na mashambulizi kutoka kwa vyombo vya serikali na visivyo vya serikali ili kuwanyamazisha na kufanya waache kutekeleza kazi zao za halali. Mashambulizi haya uhusisha vitisho, unyanyasi wa kimwili na matusi, kukamatwa kiholela na kuzuiwa pamoja na mateso kizuizini, vitisho kwa familia zao, kukataa kuandikisha mashirika ya haki za kibinadamu, mauaji yaliyopangwa na kampeni za kashfa. Mpango wa Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika ya Watetezi wa Haki za Kibinadamu (EHAHRDP) ulianzishwa kuhakikisha kuwa watetezi wa haki za kibinadamu walio hatarini wanapata usaidizi muafaka kuzuia hatari wazipatazo ili waendeleo na kazi zao za haki za kibinadamu.

Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) inawasaidia EHAHRDP kutoa usaidizi na kuwakinga watetezi wa haki za kibinadamu Afrika Mashariki EHAHRDP

inawapa kinga na ulinzi watetezi wa haki za kibinadamu walioko hatarini usaidizi wa kuhamia kwingine panapo hitajika. Wafanya jitihada kujenga uwezo wa watetezi wa haki kote kwenye ukanda huu kwa kutoa uhasishaji katika kukuza ujuzi na ufahamu wa ujuzi wa kusimamia ulinzi wao. Lengo ni kuhakikisha kwamba watetezi wa haki wanapata nafuu kutokana na hali ngumu wanazopitia na kuanza tena kazi zao za utetezi wa haki hivyo kuwafanya kuwa na uendeleo binafsi kwenye kazi zao kwa muda mrefu.

Mradi huu wa EHAHRDP wa usaidizi wa watetezi wa haki za kibinadamu walio hatarini kwenye ukanda huu hauazimii tu kuwaendeleza watu binafsi, bali pia kuwaongezea uwezo kwa jamii ya utetezi wa haki za kibinadamu kwenye ukanda kuendelea na kazi zao kwenye mazingira magumu, kwa hivyo kuzuia mipango ya kuwatishia na kuwanyamazisha.

Tunasimama na wenzetu katika wakati mgumu.

KUKUZA DEMOKRASIA

MAHIRI NA VUMILIVU

OSIEA INAS Aidia WATU
BINA FSI NA VIKUNDI
KUSHIRIKI KWENYE
MASUALA AMBAYO
YANAWAHUSU NA
KUDAI HUDUMA BORA,
UTOAJI WA HUDUMA NA
UWAJIBIKAJI KUTOKA
KWA VIONGOZI WAO
TAASISI NA SERIKALI



978-0-9838647-5-2